

NA UZAO WAKO UTAMILIKI

MLANGO WA ADUI WAKE

 Mimi, kama kawaida, nimechelewa saa moja au mbili. Mchungaji aliamka, akasema, “Sasa, ninataka kuwajulisha kwenu nyote Bw. Branham aliyechelewa.” Vema, nina mambo mengi ya kufanya kwa hiyo ni—ninachelewa tu mara mojamoja. Ila kwa wakati huu nisingeweza kuzuia jambo hilo. Ilikuwa ni kwa sababu ya hali ya hewa ambayo ilifanya hilo wakati huu. Ninaweza kuilaumu hali ya hewa na kuepuka jambo hilo. Ilibidi nilahirishe, Ndugu Rose, kidogo tu. Habari za asubuhi, Dada Rose. Basi tuna furaha kuwa nao asubuhi ya leo, Ndugu Rose na Dada Rose, na Ndugu Sharritt, na hawa ndugu wengi, ninyi watu wazuri huko nje.

² Ninasikia ya kwamba, mtu fulani ananiambia, “Inaponyesha Phoenix, kila mtu anashinda tu kitandani,” badiliko kubwa jinsi hii, mwajua. Moja ya siku hizi nitapata mlo wa bure. Wananiambia unawenza kupata mlo wa bure kila siku ambayo jua haliangazi. Nitaliangalia leo, niwafanye wauplipie huo.

³ Nilikuwa nikizungumza jana usiku, kwa kanisa fulani. Kweli sikumbuki jina lake. Na kwa hiyo tulikuwa na wakati mzuri sana, jana usiku, huko ibadani. Na huko kwa Ndugu Outlaw, na mpaka huko Tempe, nasi tuna wakati mzuri tu katika ushirika huu. Nami ninatarajia kukutana na ndugu hawa wote wahudumu kwenye mkutano huo, kwa hiyo tutakuwa na wakati kwa namna fulani wa kuketi vivi hivi huku, Ndugu Rose, na kuzungumziana. Na hilo ndilo nililolijia, ni kuwa na ushirika. Nasi tulikuwa . . . tulikuwa tukiangalia mipango yetu na kupata mahali pengi sana. Lakini niliona hii ilikuwa ndiyo nafasi kubwa sana, kwa sababu nitapata—nitapata kukutana na watu mbalimbali, kuwaona na kusonga mbele.

⁴ Wakati mwingine katika kuhubiri, kila mhudumu anaeleweka vibaya, kwa njia moja ama nyingine. Mara nyingi, watu huchukua jambo fulani unalo sema na kwa namna fulani wanainii tu . . . Linapinda kidogo kwa upande wao, kwa hiyo watalisema jinsi hiyo. Na kisha mtu anayefuata akilipata, linapinda kidogo zaidi. Muda si muda wajua, limevurugwa kabisa.

⁵ Kwa hiyo—kwa hiyo sisi, mara nyingi, katika kuhubiri, kwa namna fulani ninayashambulia madhehebu na mashirika na kadhalika. Wakati mwingine, watu wanasema basi, “Ndugu Branham anayapinga madhehebu.” Hilo ni kosa. Mimi sipingi dhehebu lolote. Lakini ni mara nyingi sana ambapo watu

wanategemea tu dhehebu hilo, unaona, na kuweka matumaini yao yote juu ya hilo badala ya juu ya Kristo.

⁶ Wanataka kuona ni wafuasi wangapi wanaoweza kuingiza kwenye dhehebu hilo. Sasa, hilo ni zuri kabisa. Mimi—mimi... Hilo ni sawa kabisa. Nafikiri kila dhehebu linapaswa kupata kila mfuasi liwezalo. Hilo ni safi kabisa. Ila unapofikia kuwachukua wasioongoka na kuweka mkazo juu ya hilo kuliko unavyoweka juu ya Roho Mtakatifu, kama vile Ndugu Rose alivyokuwa akisema hapa muda mfupi uliopita, na kadhalika, basi unapata—unawafanya watu kuwazia, “Sisi ni wafuasi wa *hili*, na tu wafuasi wa *lile*.” Hata hivyo, sisi sote ni mali ya Mungu. Unaona?

⁷ Sasa, kama nilimwona mtu akishuka kwenda mtoni katika mtumbwi. Nami ninaishi karibu na mto huko Indiana, Mto Ohio, nami niko karibu sana na maporomoko. Ni mahali pabaya sana, hayo maporomoko, kwa kuwa yatakuvunjavunja sasa hivi. Kama ukipata kutumbukia kwenye maporomoko hayo, hakuna mtumbwi ungaliweza kuyaabiri, kwa sababu ni, yako kama futi arobaini ama hamsini moja kwa moja kwenda chini, halafu mtibuko mkubwa unaibuka huko chini, amba unagonga mwamba moja kwa moja, mwamba wa huko chini ya mto. Nami nakisia vi—vi—vilele vyake, vile vilele vyeupe vya mawimbi, hufoka chini ya hayo maporomoko kwenye urefu wa futi arobaini, angalia, mahali yanapopiga chini, yanaruka juu tena. Na kisha yanaenda tu yakijifingirisha namna hiyo, kisha yanashuka chini katika mkondo wa katikati amba una kina cha futi sitini au sabini. Na mle ndani mna mzunguko wa maji amba huyazungusha *hivi*, na kuyatoa nje na kuingia chini kwenye njia ya maji. Hakuna njia kamwe ya kupona, unaona.

⁸ Mtu mmoja alienda hapa muda fulani uliopita amevaa koti la kumzuia kuzama. Waliona tu kitu hicho wakati alipoanguka, namna *hiyo*. [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] Hata koti hilo, mkondo huo wa maji ulioenda kwa kasi sana ulitmumbukiza moja kwa moja ndani. Wala kamwe hawakumpata. Kamwe haiku julikana kile kilichompata. Alining'inia juu ya miamba ama nchani kule chini, labda maili moja ama mbili huko, namna hiyo, wala hakuna njia ya kupona.

⁹ Na kama nilimwona mtu fulani akishuka kwenda mtoni katika maskini mtumbwi mdogo, ameketi pale akisoma, akiendelea, nami nikaanza kumpigia kelele, “Toka kwenye mtumbwi huo. Mtumbwi huo hautaweza kupitia kwenye viwimbi hivyo.” Sasa, si kwamba nina jambo lolote dhidi ya mtu huyo, hata kama itanibidi kumpigia kelele na kumtupia maneno makali sana. Si kwamba nina jambo lolote dhidi ya mtu huyo. Ninampenda mtu huyo, isipokuwa ninajua atavunjika-vunjika kwa kishindo. Hiyo ndiyo sababu ninampigia kelele. Kwa sababu ye ye haninii... Ni kwa sababu kweli ninampenda, ndi—ndiyo

sababu ninampigia kelele. Kama sikujali, ningesema, “Vema, heri ameondoka,” niendelee, unaona, kama sikumjali.

¹⁰ Lakini sababu ya mimi kusema mambo hayo ni kwa sababu nina juhudji juu ya Kanisa. Ni—nina juhudji kwa Kanisa la Mungu. Nami—nami ninachukia kuliona likiwa tu na nia ya kimadhehebu. Na ninajua mwelekeo huo, ya kwamba hivyo ndivyo kila kanisa limeelekea kwenye miamba, moja kwa moja namna hiyo, moja kwa moja kupitia kwenye mwelekeo huo wa kimadhehebu.

¹¹ Wazia tu juu ya uamsho katika wakati wa Walutheri, angalia mahali ulipoenda. Na mara unapofika hapo, hauinuki tena. Walutheri kamwe hawakurudi. Angalia Wamethodisti wa Wesley, hawakurudi kamwe. Waangalie Wapilgrim Holiness, Wanazarayo, hao wengine wote, Wabaptisti, Mpresbiteri. Wana uamsho, ndipo anatokea mtu akiwa na nguvu za Mungu juu yake, anaanza uamsho katika Roho. Ndipo mara mtu huyo anapoaga dunia, ndipo wanaunda dhehebu linalotokana na huo.

¹² Ni kama vile Chuo cha Biblia cha Moody, mahali pazuri, bali hapatakuwa kamwe kama vile Moody alivyokuwa amepaweka. Mnaona? Na yale mambo ambayo Moody alitetea, wao wameyaacha kwa maili milioni moja, kwa hiyo jambo ndilo hilo. Na sasa yote ni ya kiakili, wakati Moody alikuwa ameyaendesha kwa Roho, mnaona. Na kwa hiyo u—unaona hilo, katika mambo hayo.

¹³ Sasa, mara ya kwanza nilipoanza, na nikaja hapa Phoenix, miaka kadhaa iliyopita, katika uamsho wa Kipentekoste, nilikuwa na nafasi ya kuanzisha dhehebu mimi mwenywewe. Ndugu wa Mvua ya Vuli walinijia, wakasema, “Jambo ndilo hili. Hebu na tuanze. Mbona, tutakuwa wa—wakubwa kuliko hao wengine wote.”

¹⁴ Nikasema, “Rehema! Hivyo sivyo. Jambo silo—jambo silo hilo, ndugu. Mme—mmeacha nji—njia kwa mamilioni ya maili. Mungu kamwe hatariki jambo hilo.” Someni historia yenu. Someni Biblia. Kamwe hapatakuwapo na dhehebu lingine litakalotoka kwake, litakalotoka kwenye hili. Hiyo ni kweli. Hili litaunda madhehebu na kuingia katika... Liko kwenye hali ya Laodikia sasa. Lakini nitawaambia, ndugu, hakuna madhehebu mengine yaliyobarikiwa na Mungu yatakayoinuka. Hakutakuwako na kitu chochote cha hili. Tuko katika kule Kuja kwa Bwana. Mnaona? Na Mungu atachukua masazo kutoka kwenye uamsho huu mkubwa wa ekumeni, ambao unaendelea sasa, kwa ajili ya Bibi-arusi, lakini hakutakuwa na kuundwa kwa dhehebu lolote, kiroho, tena. Mnaona? Imekwisha.

¹⁵ Ninapoona ndugu zangu, ndugu wa thamani, wakiegemea upande huo, ndipo ninalikemea hilo tu kwa yote niliyo nayo. Na wakati mwengine ndugu wanasema, “Vema, Ndugu Branham anatupinga. Sisi ni ninii...” Hilo ni kosa. Jamani! Hilo—

hilo ndilo jambo lililo mbali sana na mawazo yangu, ni kumpinga mtu yeoyote. Mimi—mimi ninawatetea. Mimi ni ndugu yenu, mnaona, na ninajaribu kadiri niwezavyo. Na hiyo ndio sababu kamwe sikujiunga na dhehebu lolote lile, kusudi niweze kusimama katika pengo na kusema, “Ndugu, msininii. Hiyo siyo njia.

¹⁶ Wao wanasema, “Sisi ni Waassemblies.” Hilo ni zuri sana. Assemblies of God limekuwa baraka kubwa mno kwangu. “Sisi ni wa Foursquare.” Vema, angalia jinsi wamekuwa baraka kwangu. “Sisi ni wa Jina la Yesu.” Angalia jinsi wamekuwa baraka kwangu. “Sisi *ndio*, hao *wengine*.” Wowote wale, wote ni baraka. Wao—wao ni watu wa Mungu. Unaona? Na watu wa Mungu wamo katika hayo yote.

¹⁷ Na tunapofikia kushirikiana wenyewe, tukisema, “Sisi ni bora kidogo tu hapa kuliko Kanisa la Mungu,” unaona, ama, “Sisi ni bora zaidi kuliko wa Foursquare ama wa Jina la Yesu,” ama kitu kama hicho. Wakati sisi ni ninii tu... Huenda tusikubaliane kidogo katika mawazo. Sisi sote tulienda kula chakula cha mchana leo. Sisi sote hula sambusa ya tofauti, bali tunakula sambusa haidhuru, unaona. Wazo ndilo hilo. Kwa hiyo wazo lake, ni, kama—kama tunaweza tu kuona ushirika wetu. Kwa hiyo usiegemee kwenye dhehebu. Egemea upande wa Kalvari. Unakuifa kwa mambo haya mengine. Unaona? Nami ninaamini...

¹⁸ Hebu niseme jambo hili wakati lingali niani mwangu. Ninaamini ya kwamba dhehebu limecheza sehemu ya kutosha. Kwa kuwa, kuna mara nyingi, ndugu, ingawa tunachukia kuwazia jambo hilo, kumekuwako na mambo ambayo yameinuka mionganoni mwetu, na mambo kama hayo, ambayo yamekuwa ni uzushi. Na watu watachukua tu uzushi huo na kutawanya watu kwa njia yoyote. Na kundi la ndugu linakutana pamoja ambalo ni ninii... ambalo mimi... Ninalomaanisha ni kutoka kama walivyofanya katika siku za mwanzoni na upuuzi wa kila namna. Na—na bado tuna mambo hayo yote leo, unaona, yangali tu yanaendelea. Na watu wanaoweza kukusanyika pamoja...

¹⁹ Picha halisi ya Pentekoste, kwa maoni yangu, wakati inapofikia kwenye dhehebu, ni ka—kanisa, Ndugu Petrus, lile kanisa la Filadelfia huko Sweden. Sasa, hawajali una fundisho la namna gani, mradi tu liwe ni la Kimaandiko. Kama unataka kuliona namna *hi*, namna *ile*, ama chochote kile, mradi tu una ushirika na unaishi maisha ya kweli, safi na matakatifu. Jambo ndilo hilo. Hilo ni sawa. Na kama unataka kusema ya kwamba Yesu anakuja juu ya farasi mweupe, na huyo mwingine alisema Yeye anakuja juu ya wingu jeupe, mtarajie hivyo. Endelea tu, mradi tu unaishi maisha mema na safi na una ushirika. Njia ndio hiyo. Jambo ndilo hilo.

²⁰ Hilo, vema, sasa, hiyo ndiyo sababu moja, marafiki, ambayo niko na kundi hili la Wafanyabiashara. Kwa sababu, ninajua kuna mambo mengi sana mle ndani yanayopaswa kunyoshwa. Lakini ni ninii—ndilo bora kabisa tulilo nalo. Naam. Hiyo ni kweli. Naam. Kuna mambo mengi sana yatakayonibidi kusema. Na—nanyi, ndugu hapa watawaambia, mimi hao siwabembelezi. Niko hapa kama mtumishi wa Mungu, kuwaambia Ukweli. Nami sina budi kuwjibika kwa ajili ya jambo hilo. Hiyo ni kweli. Ndugu Rose alisema, “Hiyo ndiyo sababu tunakupenda.” Vema, hiyo—hiyo, vema, sisi hatuwezi . . . Sisi, hatuna budi kudumu na Neno hili. Unaona?

²¹ Wakati fulani tu uliopita, nafikiri, ulikuwa ninyi huko . . . nilikuwa katika nchi za ng’ambo, ama kule kisiwani mwaka jana, nao walikuwa na mukutano, na baadhi ya hao ndugu walikuwa wakijigamba katika mukutano huu mkubwa ambako walikuwa na wafanyabiashara, kote nchini. Nao walikuwa wakisema kuhusu, “Nilikuwa na mahali padogo kule pembedi. Biashara yangu haikuwa nzuri. Nami nilikuwa na wakati mbaya sana. Na haikupita muda wajua, ni—nilikuja kumpokea Kristo, na—na, loo, nina kila kitu sasa.” Sasa, hilo ni zuri. Tunathamini jambo hilo. Hilo ni zuri, bali utajiri daima haumaanishi Kristo. Hilo, unaona, nasi hatuna budi kuangalia jambo hilo. Sasa, hilo ni zuri. Unaona? Mimi . . . Sina kitu dhidi ya jambo hilo.

²² Lakini kwa namna fulani niliwafuata ndugu usiku huo. Tulishuka tukaenda kwenye moteli ambako ku—kundi letu likikuwa likikaa, na Ndugu Shakarian na sisi sote. Basi nikasema, “Vema,” nikasema, “ndugu, nitawaambia.” Nikasema, “Na—nafikiri ninyi ndugu ndio kundi zuri sana la wanaume nililowahi kukutana nalo, maishani mwangu. Lakini,” nikasema, “jambo ni kwamba,” nikasema . . .

²³ Mimi si mfuasi wa dhehebu lolote, bali mimi ni mfuasi wa ushirika huo pamoja na hao. Nina kadi yao ya ushirika, kadi pekee ninayobeba, kwa sababu linawakilisha madhehebu yote, unaona. Na hilo ndilo jambo ninalopenda. Hilo ndilo ninaloshindania.

²⁴ “Lakini,” nikasema, “jambo linalonitia wasiwasi, ni kwamba ninyi ndugu mbele ya wale watu kule chini, ambao wamestawi mara elfu moja zaidi kuliko mlivyo ninyi, na halafu mnajaribu kuwaambia ya kwamba Kristo ni utajiri. Kamwe msijaribu kuwauzia hayo.” Mnaona?

²⁵ Kamwe msijaribu kujilinganisha na ulimwengu. Acheni ulimwengu uje kwenye maeneo yetu. Msiede kwenye maeneo yao. Unaona? Unaona? Mkiondoka mwende kwenye eneo lao, kamwe hatutang’aa pamoja nao. Hata hivyo, Injili haing’ai; inameka. Hollywood hung’aa. Injili humeka. Kuna tofauti kubwa kati ya kumeka na kung’aa.

²⁶ Na kwa hiyo, sasa, nami nikasema, “Ndugu Wapentekoste wa mwanzoni waliokuwa na kitu, walijaribu kukitoa, na kuwalisha maskini, na kadhalika namna hiyo, nao wakaondoka bila kitu, unaona, kuihubiri Injili, kushirikiana.” Nikasema, “Sasa tunajaribu kujigamba kwa mali tuliyano.” Nikasema, “Ni tofauti ya jinsi gani!”

²⁷ Na maskini ndugu mmoja wa thamani, baada ya dakika chache alisimama, akaniambia, kasema “Ndugu Branham, hilo lilikuwa moja ya makosa makubwa zaidi waliyopata kufanya hao watu.”

²⁸ Nami nikasema, “Sasa, angalia, ndugu, “Sasa, angalia, ndugu, sikuwa nikijaribu kuwadokezeza kwamba watu wauze waliyano. Lakini ninajaribu tu kuwaambia hawa wafanyabiashara jambo muhimu.”

Akasema, “Hilo lilikuwa ndilo kosa kabwa kubwa, hao watu.”

²⁹ Nikasema, “Walifanya hivyo kwa Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu aliwaambia wafanye hivyo.” Roho Mtakatifu akimwambia mtu ye yote afanye jambo lolote, wewe fanya lile analokwambia ufanye.

³⁰ Naye akasema, “Vema, lilikuwa ndilo kosa lililo baya zaidi kanisa lililowahi kufanya.”

³¹ Nikasema, “Kwa nini, ndugu?” Na papo hapo mbele ya mtu nileyekuwa nikizungumza naye.

³² Akasema, “Kwa sababu, mara udhia mdogo ulipotokea mle kanisani, kulikuwa na hitilafu kati ya Wayunani na Wa—Waebrania, na kadhalika,” kasema, “watu hao hawakuwa na mahali pa kwenda. Hata hawakuwa na makazi yoyote ya kurudi huko.”

Nikasema, “Ni mapenzi ya Mungu hasa.”

Akasema, “Hayo yangeweza kuwa ni mapenzi ya Mungu?”

³³ Nikasema, “Walienda kila mahali, wakiisambaza Injili, maana hawakuwa na mahali pa kwenda.”

³⁴ Roho Mtakatifu hafanyi makosa yoyote. Hakosei kamwe. Hivyo tu. Na kama nilivyokuwa nikizungumza jana usiku, inakubidi tu kumshika Mungu, na kulichukua Neno Lake, na kulishikilia moja kwa moja. Haidhuru linakuongoza wapi, endelea tu kulifuata. Liache liendelee namna hiyo.

³⁵ Lakini hakika ni—ninaliunga mkono shirika hili la Wafanyabiashara. Na kila mukutano ninaoalikwa, daima mimi huenda kuuhutubia, kusema kila kitu niwezacho. Si kujaribu tu kujiandalia jambo fulani la kusema, ambalo lingemfurahisha mtu fulani, *Fulani*. Lakini kila wakati ninapoenda kwenye mukutano wangu, hujaribu kusoma na kuomba na kufunga, na

kusema, "Bwana Yesu, kitu gani—kitu gani ningeweza kusema ambacho kingewasaidia watu hao."

³⁶ Kila mtu anajua ya kwamba mimi si mhubiri. Mimi si msemaji. Mi—mimi ni ninii... Mtu yejote anajua hilo. Mimi si mhubiri. U—ujumbe wangu ni kuwaombea wagonjwa, na kadhalika namna hiyo. Lakini, mimi si mhubiri. Mtu yejote angejua jambo hilo, akinisikia nikihubiri. Lakini ninachosema, ninataka kutupa ngumi itakayofanya kitu fulani.

³⁷ Sio kusema, "Hivi yeje si ni m—mhubiri hodari? Yeye si anatumia sarufi yake vizuri? Yeye si ni hodari sana mimbarani?" Sitaki jambo hilo. Ni—nisingeweza kufanya jambo hilo. Mungu kamwe hakuniitia hilo.

³⁸ Lakini ninajaribu kupata jambo fulani litakalomsaidia mtu huyo, na kanisa hilo liwe kanisa bora zaidi, nilisaidie kuwa watu bora zaidi, kuliombea.

³⁹ Sasa, kwa namna fulani nilikuwa nikizungumza, nadhani, maana nimeona watu wachache wangali wakikusanyika wakiingia, nayo inanyesha. Hiyo ndiyo sababu nilikuwa nikisema mambo haya. Sasa, imepita na robo.

⁴⁰ Na sasa ninataka kumshukuru ndugu. Nimemjua Ndugu Fuller kwa muda mrefu, daima nimempenda, kutoka kwenye kilindi cha moyo wangu. Nasi tuna mambo mengi yanayofanana, Ndugu Fuller. Na kwa hiyo sisi... Nimemwona Ndugu Fuller sasa kwa miaka mingi, nami nimemjua kuwa ni mtu halisi sana wa Mungu, na ninampenda. Nami nipo hapa asubuhi ya leo kufanya ushirika. Nasikitika sana niliukosa usiku wake wakati ambao ultangazwa mahali hapa, bali lilikuwa ni jambo nisingaliweza kulizuia. Nami nina furaha kuwa hapa asubuhi ya leo, kuliona kanisa lake, zuri, jinsi ambavyo Mungu amewafanikisha na kuwabariki. Na—na kila kitu ambacho amemtendea, hakika ninathamini jambo hilo. Mungu na aendelee kumbariki, na kuibariki maskani hii, na—na ha—halmashauri ya wadhamini, mashemasi, na wafuasi wote wa kanisa. Na mkue na kufanikiwa katika neema ya Bwana, ndilo ombi langu nyenyekevu.

⁴¹ Sasa, kabla hatujaliendea Neno, hebu na tumwendee Mwandishi, kwanza. Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja kwa ajili ya maombi.

⁴² Wakati tumeketi kwa uchaji sasa penye Uwepo wa Mungu, huku vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa, je! kuna ombi moyoni mwako, kitu ambacho una haja nacho, ambacho ungetaka Bwana akupe, nipate kukukumbuka katika maombi yangu asubuhi hii hapa kanisan? Waweza kulijulisha kwa kuinua mkono wako? Liweke tu niani mwako, kwamba ni kitu gani. Bwana na ajalie kila mmoja ombi lenu.

⁴³ Baba mtakatifu na mwenye rehema, Mungu, Wewe uliyumba vitu vyote kwa Kristo Yesu, kwa ajili ya utukufu Wake, tunakuja Üweponi Mwako asubuhi ya leo tukiwa na shukrani moyoni mwetu. Na kama vile tumeendesha magari katika mvua, na upopo unavuma, mvua inanyesha, tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba Wewe utatumwagia mvua ya Mbinguni, mvua ya kiroho, mvua ya vuli na mvua ya masika, pamoa, miyoni mwetu leo.

⁴⁴ Tunaomba, Baba, ya kwamba Wewe utalibariki kanisa hili. Tunashukuru sana kwa ajili yake, kwa ajili ya mchungaji wake, kwa ajili ya kusanyiko lake, kwa ajili ya... mahali ambapo watu wanawenza kukutana kukiweko na paa juu ya kichwa chao na kitiki zuri cha kukalia.

⁴⁵ Tunarejea niani mwetu kwenye historia ya Kanisa hili la mwanzoni, Kanisa katoliki, la mwanzoni, la kimitume, na kuona jinsi walivyoketi kwenye bamba za miamba ama chochote ambacho wangeweza, kusikia Neno la Mungu, na kisha kupiga magoti sakafuni, nayo ni baridi na ina mawemawe na vumbi, na hapo wanashikana mikono kuelekea Mbinguni na kuufurahia Uwepo wa Roho Mtakatifu. Ikawapa juhudii kuu sana maishani mwao mpaka wangeenda na kuingia kwenye tundu la simba, bila hata kusogea, ila tabasamu usoni mwao, wakiangalia Mbinguni, wakijua, katika dakika chache, wangekuwa katika Uwepo Wake Yeye waliyempenda.

⁴⁶ Loo, imani ya baba zetu, ingali hai bado, pasipo kujali kifungo, moto wala upanga. Ifanye upya ndani yetu, Ee Bwana, imani kama hiyo. Tupe sisi baraka kuu ya kimitume ya Roho Mtakatifu.

⁴⁷ Kila mmoja leo aliyeinua mikono yao juu, Wewe unajua haja zao, Bwana. Unajua ni nini kilichokuwa nyuma ya mkono huo, kusudi na lengo lililokuwa katika moyo huo. Wewe pekee ndiwe unayeweza kukidhi kila haja, Bwana. Nami ninawaombea, bila kujua haja zao, bali nikiwaombea kama dua kwa ajili yao. Kama mtumishi Wako, ninaomba kwa uaminifu kwa ajili ya kila mmoja wao, ya kwamba, lolote waliloomba, naomba wapokee. Wabariki, Baba.

⁴⁸ Na sasa tunapolisoma Neno Lako, na kufundisha darasa hili la shule ya Jumapili, tuseme, asubuhi ya leo, ninaomba ya kwamba Wewe utayachukua Maneno haya na uondolee mbali kila kutokuamini, Bwana; ili kwamba, nguvu zozote za Shetani ambazo zingejaribu kuiziba, ambazo zingeizua kukua. Jalia liingie katika kila moyo, na humo lifanyike miti ya matunda ya haki, Bwana. Imani, kuleta kile ambacho Wewe umelikusudia Neno Lako kufanya, ukisema, "Halitanirudia bure, bali litatimiza kile lilichokusudiwa."

⁴⁹ Sasa, Bwana, mtakase mtumishi Wako. Neno Lako tayari limetakaswa. Na, pamoa, jalia tuweze kulilisha kundi ambalo

Roho mtakatifu alitupa tu—tulifundishe. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

⁵⁰ Sasa, kwenu ninyi mnaopenda kusoma mara nyingi, pamoja na—na Ujumbe, ningeninii... Ninawaomba, kama mngefungua katika Kitabu. Nami nina Ujumbe mdogo tu wa shule ya Jumapili, kitu kama hicho, kwa watu asubuhi ya leo.

⁵¹ Je! mnaweza kunisikia vema, huku kote, kila mahali? Niliipandisha maikrofoni hii. Nimepwelewa tu kidogo na sauti. Mimi, mara nilipofika huku, nilishikwa na homa ya mafua. Ibilisi alijaribu alivyoweza kunizua kuja hapa. Sijui. Ninaamini ya kwamba Mungu hakika ataufwagilia mkutano huu kitu fulani kikuu wakati huu, kwa kuwa Shetani amefanya kila kitu angaliweza kunizua kuja.

⁵² Lakini sasa tutasoma kutoka katika Mwanzo, mlango wa 22. Na ninyi mtakaofungua Biblia zenu, hebu tusome sehemu Yake, pamoja. Mwanzo 22, hebu tuanzie kwenye kifungu cha 9.

*Wakafika mahali pale alipoambiwa na Mungu,
Ibrahimu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari
kuni, kisha akamfunga Isaka mwanawee, akamweka juu
ya madhabahu, juu ya zile kuni.*

*Ibrahimu akanyosha mkono wake, akakitwaa kisu ili
amchinje mwanawee.*

*Ndipo Malaika wa BWANA akamwita kutoka mbinguni,
akisema, Ibrahimu! Ibrahimu! Nayee akasema, Mimi
hana.*

*Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala
usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa
unamcha Mungu, iwapo hukunizulia mwanaao, mwanaao
wa pekee.*

*Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na
tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa
pembe zake katika kichaka, ama pembe zake hasa. Basi
Ibrahimu akaenda akamtwa huyo kondoo, akamtoa
juu... awe sadaka ya kuteketewa badala ya mwanawee.*

*Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-yire, kama
watu wasemavyo hata leo. Katika mlima wa BWANA
itapatikana.*

*Malaika wa BWANA akamwita Ibrahimu mara ya pili
kutoka mbinguni,*

*Akasema, Nimeapa kwa nafsi yangu asema BWANA,...
kwa kuwa umetenda neno hili, wala hukunizulia
mwanaao, mwanaao wa pekee,*

*Katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha
nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni,*

na kama mchanga...ulioko pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa adui yake.

⁵³ Nnataka kuchukua fungu hilo la mwisho la maneno pale kwa ajili ya somo: *Na Uzao Wako Utamiliki Mlango Wa Adui Wake*. Hiyo ni ahadi ya a—ajabu.

⁵⁴ Sasa, sote tunafahamu hadithi hii, labda tumeisoma tena, tena, wakati baada ya wakati, juu ya Ibrahimu, na jinsi ambavyo Mungu alimwita atoke nchini mwake, na jinsi alivyokuwa ni mtu tu wa kawaida, hakuna kitu maalum. Bali Mungu alimwita na kumtolea ahadi.

⁵⁵ Sasa, nataka mwone ya kwamba ahadi hii ambayo Mungu alimfanya Ibrahimu haikuwa tu kwa Ibrahimu, bali ilikuwa ni kwa uzao wake baada yake. Sasa, watu wengi husema, “Loo, laiti ningalikuwa kama Ibrahimu, laiti ningalikuwa mahali ambapo Mungu alikuwa amesema nami na—na kunipa hakikisho kama alivyompa Ibrahimu, ndipo ningekuwa. Ni—ningekuwa na imani kweli, Ndugu Branham, kama tu ningeninii, kama Mungu angalikuwa amesema nami kama alivyosema na Ibrahimu.” Lakini una ahadi ile ile ambayo Ibrahimu alikuwa nayo, hiyo ni kusema, kama wewe ni Uzao wa Ibrahimu.

⁵⁶ Halafu unasema, “Lakini, Ndugu Branham, mimi ni Mmataifa. Singeweza kuwa na uzao wa Ibrahimu.”

⁵⁷ Uzao wa Ibrahimu haukuwa uzao wa maumbile ya kawaida. Ulikuwa ni Uzao wa kiroho, kwa maana tohara ya huo ilikuwa si chochote. Ile ahadi, Yeye hata alimpa hiyo kabla ya tohara. Lakini alipewa hiyo kabla ya tohara, na haikuwa ni kwa sababu alikuwa ametahiriwa na akiwa katika agano na Mungu hivyo. Ni kwa sababu kwamba Ibrahimu alimwamini Mungu.

⁵⁸ Nayo Maandiko yalisema, ya kwamba, “Tunapokufa katika Kristo, tunakuwa Uzao wa Ibrahimu.” Paulo ananena juu ya jambo hilo, “Na yule aliye Myahudi si Myahudi kwa nje, bali Myahudi kwa ndani.” Kwa hiyo, kama umezaliwa kwa Roho wa Mungu, “wewe ni Uzao wa Ibrahimu, nanyi ni warithi pamoa na Ibrahimu kulingana na ahadi.” Unaona? Kwa hiyo kila ahadi ambayo Mungu alimpa Ibrahimu ni yako, kwa sababu kiroho wewe ni Uzao wa Ibrahimu.

⁵⁹ Nawe ni Myahudi zaidi kuliko vile ungalikuwa kama ungalizaliwa katika damu ya Kiyahudi, na halafu—na halafu uwe Myahudi wa kiethodoksi katika kanisa hilo, na uwe mkanushaji wa huyu Roho Mtakatifu wa thamani na Bwana Yesu Kristo. Unaona? Wewe ni Myahudi zaidi, kwa sababu wewe ni Myahudi aliyezaliwa kwa ahadi kutoka Mbinguni, ambayo Mungu alimpa Ibrahimu, naye Ibrahimu akaikubali kwa imani, na hilo ndilo lililomfanya kile alichokuwa. Hata hivyo, Myahudi ni utengano tu, na kuvuka upande wa pili, Mwebrania, na kadhalika namna hiyo.

⁶⁰ Sasa, lakini wakati umejitenga na mambo ya ulimwengu, ukavuka ule mstari wa utengano, nawe ni msafiri katika nchi ya kigeni, nchi kama ile usiyokuwamo, hapo mwanzo, pamoja na watu ambao kamwe hujawahi kushirikiana nao hapo mwanzoni, ndipo unakuwa Myahudi wa kiroho. Kwa sababu, namna ile ile ya Ibrahimu, kwa imani, aliondoka nchini mwake, akawaacha watu wake, akaingia katika nchi ya kigeni ya watu wageni. Umewaacha watu wako, ukauacha ulimwengu nyuma, ukawaacha wenzako nyuma, ukavuka, kwa Damu ya Yesu Kristo, nanyi ni wasafiri, mkiutafuta Mji Ambao Mwenye Kuujenga na Mwenye Kuubuni ni Mungu, kama vile Ibrahimu alivyokuwa. Wasafiri, pamoja Naye, mkiishi hemani, makanisani, wenyeji pamoja nasi wa Ufalme wa Mbinguni, warithi wa vitu vyote kwa Yesu Kristo. Unaona? Tumevuka ng'ambo ya pili, tumetenganishwa.

⁶¹ Sasa, Ibrahimu, ahadi imefanywa kwa Ibrahimu na Uzao wake baada yake. Sasa, Mungu alimpa Ibrahimu ahadi hii, ya Uzao wake, utamiliki mlango wa adui wake akiisha kumjaribu Ibrahimu, kumpima Ibrahimu. Sasa, baada ya kuja kwa majaribio, ndipo . . .

⁶² Ibrahimu alikuwa tayari ameongoka, tungekuita, kutoka kwenye upagani akaingia kwa Mungu. Na ndipo Mungu alikuwa amempa, kama ishara ya Roho Mtakatifu, tohara. Ndipo, baada ya tohara, ndipo ukaja wakati wa kujaribiwa.

⁶³ Mfano mzuri sana hapa wa Kanisa, ambapo, baada ya sisi kuokolewa, ndipo tunapewa muhuri wa tohara iliyohidiwa, ambayo si ya mwili, bali ya Roho. Naye Roho Mtakatifu ndiye tohara yetu. Ndiye kisu kikali cha Mungu. Kinatenganisha na kukatilia mbali nyama ya ziada, ya ulimwengu, kutoka kwetu. Neno la Mungu, kali kuliko upanga ukatao kuwili! Kwa hiyo, unaona, linalo moja kwa moja tena. Neno la Mungu ndicho kitu ambacho Roho Mtakatifu hutumia; siyo kanuni za imani, si madhehebu. Bali Neno ndilo linalotutenganisha na mambo ya ulimwengu. Linakatilia mbali mawazo yetu na kadhalika, na kutuweka wakfu kabisa kwa Mungu.

⁶⁴ Yesu alisema, "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu." Jambo ndilo hilo. Ndipo, si neno lako. Ni Neno Lake. Ndipo, unaona, "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu, mngeweza kuomba mtakalo." A-ha. Unaona? Jambo ni kwamba, huneni neno lako mwenyewe. Unanena Neno Lake.

⁶⁵ Kwa hiyo basi Roho Mtakatifu Ndiye anayelichukua Neno la Mungu na kututenga na mambo haya ya ulimwengu, unaona, tohara, kukatilia mbali. Ndipo unapitia kwenye wakati wa majaribio.

⁶⁶ Sasa, Ibrahimu, baada ya ye ye kuitwa atoke, nchi ya Wakaldayo, mji wa Uru, akawa msafiri, mgeni. Na ndipo

Mungu akamwita, baada ya yeye kuthibitishwa ya kwamba ataendelea na kumchukua Mungu katika Neno Lake. Ndipo, kile Mungu alichofanya wakati huo, kilikuwa ni kumpa ishara, ya kwamba alikuwa amemkubali, Naye akamtahiri. Naye akamtahiri Ishmaeli na nyumba yake yote.

⁶⁷ Na sasa unaona, wakati—wakati unapoitwa utoke, kwanza unapitia kwenye majaribio, kuona kama kweli utaendelea. Ndipo Mungu anakupa Roho Mtakatifu, ambaye ni ishara ya kwamba Yeye ameikubali imani yako unayokiri kuwa nayo ndani Yake. Mnanielewa sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye ataikubali.

⁶⁸ Sasa, nilikuwa ninaongea na... Huenda kukawa na ndugu wa thamani wa Kibaptisti wanaoketi hapa. Na kila mtu anajua ya kwamba nilitoka kwenye kanisa la Kibaptisti. Nilikuwa nikizungumza na ndugu yangu Mbaptisti. Naye akaniambia, “Ndugu Branham?” Yeye alikuwa ni Daktari wa Uungu, mtu mzuri, Mkristo halisi. Akasema, “Lakini, Ndugu Branham, unapata wapi kwamba ubatizo wa Roho mtakatifu ni kitu chochote tofauti na imani katika Kristo Yesu?”

Nikasema, “Ni tofauti, ndugu yangu mpendwa.”

⁶⁹ Akasema, “Hivi huoni ya kwamba unapompokea Kristo, unampokea Roho Mtakatifu?”

⁷⁰ Nikasema, “Kweli. Lakini,” nikasema, “unaona, unakiri tu ya kwamba umempokea Kristo, mpaka Yeye atakapotambua jambo hilo.”

⁷¹ Akasema, “Ndugu Branham, Ibrahimu alimwamini Mungu, naye akahesabiwa kwamba ana haki.”

⁷² Nikasema, “Ndiyo. Lakini Mungu alimpa ishara, kwamba Yeye alikuwa ameipokea imani yake, wakati alipompa muhuri wa tohara, kwamba Yeye alikuwa ameitambua imani yake.” Amina.

⁷³ Sasa, tunapompokea Kristo kama Mwokozi wetu, halafu, kama sisi ni waaminifu katika jambo hilo, basi Mungu hutupa ishara, ya kwamba Yeye ameipokea imani yetu katika Kristo, kwa kutupa muhuri wa tohara, ambao ni Roho Mtakatifu. Huo ndio muhuri wa tohara. “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye kwa Yeye mmetiwa muhuri hata Siku ya Ukombozi wenu.” Si hata kwenye mkutano huo mwininge; bali hata Siku ya Ukombozi wenu. Hiyo ni kweli, Waefeso 4:30. Sasa, hivyo ndivyo tunavyompokea Roho Mtakatifu.

⁷⁴ Sasa, kama ukisema, “Loo, mimi ni mwaminio,” wala Mungu kamwe hajakupa Roho Mtakatifu bado, Yeye kamwe hajaitambua. Unakiri tu ya kwamba unaamini. Lakini wakati mashaka yote... Sisemi wewe si mwaminio sasa. Kwa sehemu fulani, wewe ni mwaminio.

⁷⁵ Lakini wakati Mungu amepata majaliwa, umepata majaliwa Kwake, hasa, na anakutambua kuwa mtoto Wake, Naye anaujua moyo wako, na anaona uaminifu wako, anajua mambo yote yameondolewa mbali nawe. Ndipo Yeye anakutia muhuri kukuizingiza katika Ufalme wa Mungu, kwa Roho Mtakatifu, akiuthibitishia ulimwengu ya kwamba Yeye amekubali imani unayokiri kwamba unayo ndani Yake. Mnalifahamu sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

⁷⁶ Sasa, mara baada ya jambo hilo, jaribio linakuja. "Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kurudiwa kwanza, kujaribiwa."

⁷⁷ Yesu, mara alipopokea utimilifu wa Roho, pale mtoni, wakati Yohana alipombatiza, mara ibilisi alimpeleka nyikani, apate kuititia wakati wa majaribio. Bali wakati alipolichukua Neno la Mungu na kumshinda ibilisi, "Imeandikwa. Imeandikwa," Yeye alirudi akitokea huko basi akiwa tayari kwa ajili ya huduma Yake.

⁷⁸ Na hivyo ndivyo Mungu aliyoyomfanyia Ibrahimu. Sasa, Mungu, baada ya kumwita atoke katika nchi yake, naye akajitenga na nchi yake, watu wake, na halafu Mungu akampa muhuri wa tohara, kisha akampa mwana. Ndipo alishuka akaenda kwenye lile jaribio la mwisho, moja kwa moja kufikia wakati ilipombidi kumtoa mwanawe Isaka kwa ajili ya dhabihu. Ndipo akasema, "Kwa maana hukunizulia mwanao wa pekee, ninajua ya kwamba unanipenda Mimi." Yeye alimpa jaribio hilo.

⁷⁹ Ndipo mara baada ya jambo hilo, vita vilishindwa basi, Yeye akasema, "Na uzao wako utamiliki lango la adui yake." Amina. Ninapenda jambo hilo. "Atamiliki lango la adui yake." Tutafikia kwenye jambo hilo la mwisho katika dakika chache tu, Bwana akipenda. Sasa aliona jambo hili, Ibrahimu ni mwaminifu. Baada ya kumwona Ibrahimu alikuwa ni mwaminifu, basi alimpa ahadi ya kumiliki lango la adui.

⁸⁰ Sasa hapo, mara nyingi, pale ambapo wengi wetu Wapentekoste tumefanya kosa, na kuwazia, "Vema, Roho Mtakatifu amemwagwa juu yangu. Utukufu kwa Mungu! Hayo tu ndiyo yanayonipasa kuwa nayo." La, bwana. Wakati huo ndio kwanza tu umeanza. Wewe, si wakati huo. Ni jaribio lako na kupimwa kwako.

⁸¹ Ni kama tu tunavyoona katika—katika, humu katika A—A—Agano la Kale; kujaribiwa, kupimwa, kisha kumweka mwana mahali pake. Kufanywa mwana mwenye mamlaka, kumweka mwana baada ya yeye kuwa ni mwana tayari, amezaliwa katika familia hiyo. Yeye ni mwana, ndipo angejaribiwa na kurudiwa, na kulelewa na walimu, na kuona jinsi anavyokuwa. Ndipo anawekwa mahali pake akiwa sawa, akiwa karibu sawa, na baba yake.

⁸² Sasa hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Tumekuwa na karibu miaka arobaini ya kujaribiwa kwa Pentekoste, ama zaidi, unaona, kulijaribu kanisa, kuona kama watastahimili, ama la. Kuona vile ninyi . . . Na, unaona, hapo ndipo ninapolipata tena. Badala ya kushikilia msalabani na kwa Neno, na kusonga mbele, tunajifananisha na ulimwengu, tukianguka *hivi*, ama kuanguka *hivi*, ama kujifananisha na *hili*.

⁸³ Kama ambayyo sikuzote nimezungumza kwa ukali sana dhidi ya watu katika mwelekeo huu wa kisasa siku hizi, wanawake wakikata nywele zao, na—na wanaume wakifanya maovu na kadhalika, na kuva tu nguo chafu na kadhalika. Ninapata ukosoaji mkubwa sana juu ya jambo hilo. Lakini ni kitu gani? Ni kujaribu kuliokoa kanisa hilo. Ni kujaribu kuwaleta *hapa* juu, kwenye Neno la Mungu, bila kujali kile ulimwengu mwininge unasema juu Yake. Dumu na Neno la Mungu. Amina. Unaona? Unaona?

⁸⁴ Jambo lenyewe ni kwamba, kama nilivyokuwa nikisema jana usiku, Wapentekoste wanangojea upepo wa nguvu unaovuma kwa kasi, bali walishindwa kuisikia ile Sauti ndogo tulivu. Unaona? Kwamba, ni vibaya kufanya mambo hayo. Wanawazia, “Mradi tu upepo unaenda kasi, vema.”

⁸⁵ Lakini hilo halikuuvutia usikivu wa nabii. Huo upepo ulioenda kasi kamwe haukumsumbuu nabii Eliya pangoni. Zile ngurumo zenyе nguvu na radi, na mvua kumwagika, kamwe havikumvutia, vyote. Lakini kilichomshitusha sana kilikuwa ni ile sauti ndogo tulivu, kile kitu kinachonena mle ndani. “Neno Langu ni Kweli. Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe kweli.” Hilo ndilo lililomvutia nabii huyo. Unaona?

⁸⁶ Na ingali itafanya hivyo. Neno la Mungu daima huivutia nia ya kiroho, kwa maana ni nia ya Kristo ndani yako, ambayo inajua ya kwamba Neno hilo ni kweli.

⁸⁷ Nawe unapitia katika wakati wa kujaribiwa. Kanisa linapitia wakati wa kujaribiwa. Kila mtu binafsi anapitia katika wakati wa kujaribiwa kabla ya kuweza kumiliki lango la adui. Ibrahimu alipitia hilo. Kristo alipitia hilo. Baada ya Kristo kujazwa na Roho Mtakatifu, pale kwenye mto Yordani, Yeye alipitia katika wakati wa majaribio. Baada ya Ibrahimu kuitwa atoke, akawekwa katika nchi yake ambamo alikuwa awe mgeni, kisha kapewa tohara, na Mungu akakutana naye, wakati baada ya wakati, hata hivyo ilimbidi kupitia katika wakati wa kujaribiwa. Kila uzao wa Ibrahimu hupitia kwenye jambo lile lile, Ibrahimu na Uzao Wake.

⁸⁸ Dhehebu, kanisa, hiyo ndiyo sababu tunaona madhehebu yetu yakiangukia kando ya njia, ni kwa sababu inapofikia kwenye jaribio. Jaribio gani? Neno la Mungu. Hilo ndilo jaribio. Neno la Mungu ndilo jaribio. Je! tutafanya yale kundi la watu

linayosema tufanye, ama tutafanya yale Mungu anayosema tufanye? Tofauti ndiyo hiyo.

⁸⁹ Hilo hapo likaja, siku za Dwight Moody, siku za Finney, Sankey, Knox, Calvin, Spurgeon, hao wengine wote, hao watu wa kiroho, madhehebu yaliwafuata. Walilichukua kundi la watu kule nyuma waliojipenyeza mle, kila mmoja akiamini jambo *hili na lile*, na kuongezea kidogo *hapa*, na kutoa kidogo *pale*, na kuongezea kidogo *hapa*, mpaka hatimaye wakaunda dhehebu kutoka kwake.

⁹⁰ Na wanapofanya jambo hilo, mwaminio halisi na wa kweli, Mungu huja hapo moja kwa moja na kumchukua maskini mtu fulani, mnyenyeketu, anakivunjilia kitu hicho vipandevipande. Kweli. Amefanya hivyo daima. Mungu habadiliki. Anakirarua tu kitu hicho vipandevipande, watu wenye nia ya kiroho ambao watadumu moja kwa moja na Neno hilo.

⁹¹ Hebu niwaambie. Nina barua nyumbani, ya moja ya makanisa yaliyo mazuri sana, madhehebu makubwa katika uamsho wa Kipentekoste. Maskini mwanamke huyo aliyevunjika moyo aliniandikia barua. Naye alisema, “Ndugu Branham, nilikuwa nina nywele ndefu na nilikuwa na fundo la nywele zilizosokotwa nyuma ya kichwa changu.” Akasema, “Na ninii... Mume wangu alizipenda.” Halafu akasema, “Tulihama toka kwenye mji ambapo tulikuwa na kanisa lililokuwa la kiroho kweli, kwenda ambako kanisa hili kubwa, kanisa la kwanza la mji huo.” Kisha akasema, “Tulipoingia mle, dada wote wa Kipentekoste walikuwa wamekata nywele zao.” Kisha akasema, “Walinishambulia juu ya jambo hilo. Nikasema, ‘La, la. Ninaamini Biblia inasema tusifanye jambo hilo; ni aibu kufanya hivyo.’” Na kwa hiyo akasema tu, “Nao waliendelea... Wangemcheka, waseme, ‘Aisee, gu-gurundumu lako la nyuma limetoboka, lako la spea,’ na yote jinsi hiyo. Ndipo wakamwingilia mume wangu, hivi kwamba, mpaka akanilazimisha kuzikata nywele zangu.” Naye akasema, “Nimehukumiwa, tangu wakati huo.”

⁹² Wazia jambo hilo, kanisa la Kipentekoste linalopaswa kulitetea Neno la Mungu! Huko ndiko dhehebu lako linakowapeleka. Kweli. Wanashindwa kusikia sauti hiyo ndogo tulivu ya Neno, inayowaita kwenye kweli. Wote wanasililiza uvumi wa pepo kali zikienda kasi, na kupiga makelele kwingi na kucheza dansi, wakisema wana nguvu. Hilo ni sawa. Ninaamini katika jambo hilo, pia. Lakini, ndugu, wakati unapoweza kucheza na kupaza sauti, kisha unageuka na kukana Neno la Mungu, na kuishi kama ulimwengu, kuna kasoro fulani mahali fulani. Kweli.

⁹³ Roho wa Mungu hushuka chini, ile Sauti ndogo tulivu, na kukuongoza moja kwa moja hadi Kalvari, ambapo tumekufa, na uhai wetu umefichwa katika Mungu kwa njia ya Kristo, na

kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Ndipo, Neno hilo peke yake linaishi pale. “Ndipo mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo nanyi mtapewa.” Hiyo hapo tofauti.

⁹⁴ Natumaini sionekani kwenu kama mkereketwa wa dini. Kama ndivyo nilivyo, si—si—sijui hayo. Ni—ninaamini ya kwamba Neno la Mungu ni Kweli, Nalo halina budi kukaa papa hapa. Na kama likikaa hapa, litajionyesha Lenyewe kwa nje. Halina budi kujionyesha! Maisha yako, utu wako wote, utakuwa ni tofauti.

⁹⁵ Kwa hiyo wakati Mungu alipompa Ibrahimu jaribio, alipita, asilimia mia moja. Na angeninii...

⁹⁶ Mungu hawesi kulipa dhehebu jaribio, kwa sababu lote limechanganyikiwa. Mungu halishughulikii dhehebu namna hiyo. Hayashughulikii mataifa katika jamii ya Kimataifa. “Aliwachukua watu kutoka katika Mataifa.” Israeli, Yeye alichukua taifa. Lakini, kutoka katika Mataifa, “Yeye alichukua watu kutoka katika Mataifa kwa ajili ya Jina Lake.” Kwa hiyo, unaona, si dhehe—... Si dhehebu. Humtoa mtu binafsi kutoka kwa Mataifa.

⁹⁷ Ndipo jaribio linapokuja, unaona linalotukia? Tilitoka tukaja kwenye kuhesabiwa haki. Tulipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu katika uamsho wa kipentekoste. Lakini inapofikia kwenye wakati wa kujaribiwa, tunawachukua wasomi hodari, tunataka kuwa kama ulimwengu, kama tu ilivyokuwa katika siku za uamsho wa Wesley na hao wengine wote. Wanaenda shulen. Wana—wanajifunza sayansi. Nao wanajifunza mambo haya mengine yote yanayoambatana na elimu. Nao wanajaribu kujifunza saikolojia. “Jambo tu lilio bora kuliko mambo yote, vema, usijaribu kusema *hili*. Acha wafanye *hivi* na *vile*. Kwa sababu itaninii...” Unaona, unakusanya na kujenga. Ni—ni—nia yako ni mbaya. Kusudi lako ni baya. Unaunda dhehebu badala ya kujenga ukielekea Kalvari. Unawezaje kujenga ukielekea Kalvari, pasipo kuja kwa njia ya Neno?

⁹⁸ “Kwa kuwa tunaoshwa kwa maji ya Neno.” “Mkikaa ndani Yangu na Maneno Yangu yakae ndani yenu, basi ombeni mtakalo.”

⁹⁹ Hapo ndipo tunaona kushindwa kwa uamsho wa Kipentekoste, kwa sababu wanaondoka kwenye Neno. Neno litasema jambo moja; watajaribu kulifanya dhehebu hilo liingie pale mahali fulani. Nao wataondoka moja kwa moja kutoka kwenye hilo Neno, na kuungana moja kwa moja na dhehebu. Nanyi mnaona mahali ambako limeelekeea? Ni karibu kama makanisa hayo mengine. Lakini basi tunacheza na kupaza sauti, na kunena kwa lugha, na kuruka-ruka, hayo yote ni sawa. Dhehebu lao ni sawa. Natumaini nilijieleza vizuri. Lakini jambo ni kwamba, hiyo Sauti ndogo tulivu ya Neno inayonena. Hiyo ndiyo.

¹⁰⁰ Unapitia kwenye jaribio. Mungu anakujaribu kama alivyomfanya Ibrahimu. Yeye hujaribu Uzao wa Ibrahimu, baada yake. Na sasa, sababu ya sisi kutoumiliki mlango wa adui, sababu ya kuwapo na mambo mengi sana mionganini mwetu, ni kwa sababu hatuwezi kustahimili jaribio. Na hebu niwaambie jambo fulani, jaribio la Neno ni zuri.

¹⁰¹ Sababu ya sisi kutokuwa na ninii, wala kamwe hututakuwa na ninii... katika dhehebu. Nafikiri Pentekoste ina dhehebu zuri. Baadhi ya watu walio bora sana nili-... wanaokaa... wanaoishi juu ya uso wa dunia, ni wafuasi wa hayo—hayo madhehebu.

¹⁰² Assemblies of God, nina marafiki mle. Jamani! Ndugu fulani moja kwa moja huko Indiana, nitafanya, nitafanya mkutano, ninaamini, mara, mara moja. Ndugu Roy Weed, yeye ni mkuu wa wilaya ya jimbo la Indiana. Ninaamini huyo ni mtu mcha Mungu. Hata hivyo, yeye ni mkuu wa wilaya wa Assemblies of God.

¹⁰³ Foursquare, loo, jamani, ni wangapi! Ralph McPherson na wengi wa hao ndugu, ambao ni wacha Mungu, hakuna doa maishani mwao. Wao ni watu wazuri.

¹⁰⁴ Huko kwa wa Umoja, jinsi wanavyojiita, Umoja. Ama, sasa, sidhani... Wanaliita kanisa la Jina la Yesu. Jack Moore, nikitaja tu moja kutoka kwenye... Kuna mamia ya hao, watu wazuri, watu wema, watu wacha Mungu.

¹⁰⁵ Lakini jambo ni kwamba, ndugu, ni hili, wakati unapodumu kwenye dhehebu hilo. Unaona? Mungu huyachukulia madhehebu hayo, na-na kila moja limeanguka. Yaangalie, mambo ya ulimwengu yakitambaa kuingia ndani. Waangalie wanawake wao. Waangalie wanaume wao. Angalia hali zao. Ningeweza kuwaonyesha, watu wa Assemblies of God walio na mashemasi kwenye halmashauri yao, ambao wameoa mara mbili ama tatu, wahubiri wakifanya maovu. Wanawake waliokata nywele zao, wanaovaa kaptura, vipodozi, na wangali wanakirii wana Roho Mtakatifu, wakitegemea ushuhuda wa kunena kwa lugha, ama kurukaruka, au kupaza sauti.

¹⁰⁶ Wanashindwa na ile Sauti ndogo tulivu ya Neno. Neno hilo hukupatanisha na msalaba. Hapo ndipo lilipo. Hiyo ndiyo sababu hatuna manabii halisi kanisani siku hizi, kama vile Agabo.

¹⁰⁷ Hiyo ndiyo sababu, kanisa siku hizi, ni vigumu kwa—kwao kuheshimu kunena kwa lugha wakati mtu fulani anaponena, kwa sababu wamesikia uongo mwingi sana pamoja na upuuzi, mpaka hawajui ukweli ni nini ama uongo katika hayo.

¹⁰⁸ Fasiri hizo ni madanganyo tu, mtu anasema tu jambo fulani kwa sababu anajisikia kuongozwa. Hiyo si tafsiri. Tafasiri; si mtu kusimama na kunena kwa lugha, mwingine anasimama katika dakika chache na kufasiri yale aliyosema. Wakati mtu

anapozungumza, huyo mwengine anafasiri papo hapo, akisema neno kwa neno, tamshi lile lile, kila kitu vile vile. Huenda ikawa mtu *huyu* anatabiri, bali si fasiri. Baadhi yao, sauti ya aina *hii* ikitoa jambo fulani, *hii* hapa nyuma ikitoa jambo tofauti. Na wengine wasema maneno kumi, mwengine anasema maneno hamsini nyuma yake, ati ni tafsiri.

¹⁰⁹ *Kutafsiri* maana yake ni “kusema, neno kwa neno.” Kama ni Neno la Mungu, linapaswa kuja, neno kwa neno; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni. Hivyo ndivyo Neno linavyopaswa kuja.

¹¹⁰ Lakini tumeona kitu gani? Upuuzi mwangi sana! Nao walifanya hivyo, kwa utaratibu, badala ya kudumu na Neno, waliliweka hilo pale chini. Mara mtu fulani alipofanya hivyo, walimwita Mpentekoste. Nanyi mnajua linalotukia.

¹¹¹ Majaribu yanapokuja, wakati wa kujaribiwa, ndipo Mbegu inaanza, inaonyesha kwamba Mbegu ni ipi na ni ipi isiyo. Sasa, haidhuru ni jambo gani lililotukia, Ibrahimu alidumu na Neno, ile ahadi.

¹¹² Lakini leo dhehebu haliwezi kufanya jambo hilo. Na baadhi yenu ninyi ndugu wa thamani ambaa ni wafuasi wa madhehebu hayo, hebu msikubaliane nao siku moja, mnajua mahali mmeenda. Ni wangapi wenu?

¹¹³ Sisemi, katika jengo hili sasa, ila ni wangapi wamekuwa kwenye chumba changu cha kusomea, ni wangapi wamekuwa pamoja nami, wanasema, “Ndugu Branham, tunajua hiyo ni Kweli. Lakini kama tukifukuzwa hapa, tutafanya nini?”

¹¹⁴ Ndugu, ati tutafanya nini? Shikilia Kalvari, shikilia ile ahadi, shikilia msalaba, haidhuru.

¹¹⁵ Na mle ndani, wana baadhi ya watu walio wazuri sana. Unaona? Lakini kile ninachojaribu kufanya, ni kusema, hilo halina budi kushindwa. Daima limeshindwa na daima litashindwa. Lakini ni, kama ukishindwa ama usishindwe, kwa Mungu, timiza Neno la Mungu na ahadi Yake, kwanza. Utajaribiwa Nalo.

¹¹⁶ Utatia sahihi makaratasi, kwamba utafanya *hivi* ama utafanya *vile*. Hata dhidi ya Neno, bado utatia sahihi. Hiyo ni kweli. Moyoni mwako, unajua ni kosa. Hiyo ni ile Sauti ndogo tulivu ikinena, lile Neno. Si ajabu hatuwezi kusonga mbele, kwa sababu ya kile kimetendeka. Ulijitenga na ile Sauti ndogo tulivu. Ulikimbia nje upesi sana. Mungu alikuwa akikuuta, bali ulikimbia nje upesi sana, kwa sababu ngurumo zilinguruma, na radi ikimulika, mlima ukatetemeka.

¹¹⁷ Haikumtikisa Eliya, yule nabii. Yeye alitaka ile Sauti, kwanza. Akasema, “Nitakaa papa hapa.”

¹¹⁸ Wengi sana siku hizi, walianza, ibada za uponyaji, kujilinganisha kimwili, kila namna ya mambo, na mihemuko

ambayo hata haionekani katika Neno la Mungu. Hiyo ni kweli. Ni kitu gani? Inatupasa kuimba ule wimbo, “Wao wamnganjeao Bwana. Nijalie midhili majivuno yangu na niliite Jina Lako. Jalia ningoje, Bwana, mpaka nitakaposikia hiyo Sauti ndogo tulivu.” Na Sauti hiyo itakuwa ni Sauti ya Kimaandiko. Itanena sawasawa kulingana kabisa na Neno. Amina. Vema.

¹¹⁹ Akapatikana, Ibrahimu akiisha kuwekwa, kuitwa atoke, kutengwa na wapendwa wake, na familia yake, na nyumba yake, na jamii yake, akaenda kwenye nchi ya kigeni. Kwa imani alifanya hivyo. Halafu, kwa sababu alifanya hivyo, Mungu alimpa tohara, kuthibitisha ya kwamba ye ye aliкуwa ni mwana wa Mungu, ya kwamba alimwamini kwa maana aliкуwa akiamini ile ahadi. Hata hivyo, hakuweza, hakuliona kimaumbile, bali alikiri, “Chochote kinyume na Neno la Mungu kilikuwa ni uongo.” Haidhuru ni ushahidi kiasi gani uliotolewa, ingali ni uongo.

¹²⁰ Ninachukia kusema jambo hili, bali itanibidi kulisema. Angalia. Na wakati mnapowachukua wanawake, nitasema jambo hilo kama kitu kimoja kinachoonekana, tunachoweza kuona, wanaodai kuwa na Roho Mtakatifu, wala hawana adabu ya kutosha ku—kuachilia nywele zao zikue, kuna kasoro fulani mahali fulani. Mwanamke atakayevaa vazi limpasalo mwanamume, na kulivaa, wakati Biblia inaposema, “Ni chukizo kwa—kwa Mungu, kwa mwanamke kuva vazi limpasalo mwanamume.” Halafu basi unadai kuwa na Roho Mtakatifu na unafanya hivyo?

¹²¹ Nilizungumza juu ya jambo hilo siku moja huko Oregon. Kuna mwanamke aliyeninandikia barua kubwa mno. Akasema, “Ndugu Branham, una huduma ya ajabu, bali hakika unaiangamiza.” Akasema, “Sasa, vipi kuhusu...” Kasema, “Ninavaa maovaroli wakati wote.” Kasema, “Vipi kuhusu kutoka kwenda bustanini kuchuna ki—kidogo bustanini, na huku umevaa rinda. Hivi hudhani ingeonekana vizuri zaidi ukiwa umevaa maovaroli kuliko ingalikuwa, ama dangirizi, ama chochote kile, kuliko kuva rinda?” Kisha akasema, “Angalia, mimi hupanda farasi huko milimani pamoja na wavulana wakati wanapoenda kuwachunga ng’ombe, na,” kasema, “Mimi huingia kwenye eneo lililojaa mbu.” Kasema, “Sasa, nikiwa ni—nimevaa rinda, wangenila kabisa. Nikiwa na ovaroli hawanisumbui.”

¹²² Nikasema, “Hayo ni membamba kuliko mchuzi uliotengenezwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa. Rehem! Halina Neno moja la Mungu kwake. Hayo ni maomi yako mwenyewe.”

¹²³ Mungu alisema, “Kila neno na liwe uongo, na Lake liwe ni kweli.” Mke wangu huvaa rinda. Yeye huchuma bustanini. Hana shida nayo. Na, kwa hali yoyote, mwanamke hana shughuli kuwa pamoja na kundi la wanaume huko nje, akiwachunga ng’ombe,

kwa vyovyote vile. Anapaswa kuwa jikoni ambako ndiko mahali pake. Hiyo ni kweli.

¹²⁴ Wanajaribu tu kupata udhuru, bali haupo. Neno la Mungu ni dhahiri, na mwanamke aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu atakuwa hivyo. Na mwanamume aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu hatamruhusu mkewe afanye hivyo. Yeye alisema nini? “Yeye anayechukua, anayekata nywele zake, yuaabisha kichwa chake.” Na mume wake ndiye kichwa chake. Yeye hana heshima.

¹²⁵ Afadhalni nifunge mdomo. Vema. Sasa, unaona, unaona, hilo limetosha. Mnajua ninalozungumzia.

¹²⁶ Sisemi hilo kwa ukorofi. Kama nikisema hilo kwa ukorofi, Mungu aurehemu moyo wangu wenye dhambi; hebu nishuke nije hapa madhabahuni, nikatubu.

¹²⁷ Ninasema jambo hilo kwa sababu, enyi marafiki, ninawapenda. Nami ninajaribu kuwaambia lililo kweli, na hilo ni Neno la Mungu. Inatupasa kusikia hiyo Sauti ndogo ya Mungu, kufikia kiwango cha Neno. Tunapitia wakati wa majaribio. Haleluya!

¹²⁸ Je! ultambua ya kwamba baada ya wakati huo wa majaribio kujua, yale mafundisho ya yule mwana aliyezaliwa katika familia ya kimadhehebu? Kama aliystahimili majaribio na kudumu na mapenzi ya baba yake, basi huyo mvulana alitolewa nje na kuvalishwa vazi, ndipo kuna sherehe inayofanyika. Ndipo mvulana huyo aliwekwa basi katika familia aliyozaaliwa.

¹²⁹ Hiyo ndiyo shida ya Wapentekoste wetu siku hizi. Wao wanaruka tu *hapa na pale*, na madhehebu yetu yangewavuta *huku na kule*. Hawadumu na Neno.

¹³⁰ Kama utadumu na Neno, basi Mungu, akiona, “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu,” Lake, Yeye hawezikulikana. Ni Neno Lake. Ndipo kutakuwako na wakati, wakati fulani, utakapotolewa nje na kuwekwa kando, na kupewa kitu ambacho ni halisi, haleluya, nguvu za Mwenyezi Mungu.

¹³¹ Jambo ambalo, Mungu anawangojea watoto Wake, bali kabisa hawatajirekebisha, wanapofikia kwenye ule wakati wa majaribio. Je! utalikubali? “Vema, kanisa litanifukuza.” Vema. Haya basi. Basi, nenda. Huo si Uzao wa Ibrahimu. Uzao wa Ibrahimu haufanyi hivyo.

¹³² Uzao wa Ibrahimu! Sasa, sijali ni kitu gani kilichokuja kinyume na Ibrahimu, yeye alidumu moja kwa moja na hilo Neno la ahadi, alidumu tu moja kwa moja nalo. Haidhuru Sara alikuja, jinsi wengine walivyokuja, watu mbalimbali walivyokuja, kila kitu, yeye aliyahesabu kana kwamba hayakuwa. Yeye alitazama, aliamini ya kwamba angeweza kuiona ile ahadi, kwa kuwa Mungu alimwahidia, na ilikuwa ni hayo tu hakukuwa na la zaidi. Lilikuwa ni Neno la Mungu, lililodumu moja kwa moja ndani yake.

¹³³ Ndipo akampa lile jaribio la mwisho. “Nitampa sehemu maradufu, na kumjaribu.” Sasa, ye ye tayari ana mwana. Anaona kwamba ana huyo. “Ila sasa nitamwambia, ‘Mpandishe huyo mwana ukamwue.’ Na kumwacha mwana huyo, wakati alipoona... Je! atamwua huyo mwana? Nitamjaribu sasa.”

¹³⁴ Ibrahim, akiwa mwaminifu kwa Neno! Vipi, wakati unapoipokea ile ahadi, utakomeshaje kitu hicho? Vipi, utakikomeshaje?

¹³⁵ “Utatarajiaje kuwa baba wa mataifa, nawe huyu hapa ukiwa na umri wa miaka mia moja na kumi na mitano sasa? Ibra-... Maskini Isaka, ana umri wa karibu miaka kumi na minne, kumi na mitano. Utakuwaje baba wa mataifa wakati ukiwa na umri wa miaka mia moja na kumi na mitano? Huyu hapa mtoto wako wa pekee, nawe unaangamiza thibitisho lako la pekee ulilo nalo.” Amina.

¹³⁶ “Nitafauluje kama nikitoka katika dhehebu langu? Nitafauluje kama nikifanya jambo *hili*?” Loo, sikiliza ile Sauti ndogo tulivu na uje kwenye Neno, lile Neno.

¹³⁷ Unasema, “Nilisikia sauti ikiniambia *hivi*.” Kama ni kinyume cha Neno, haikuwa Sauti ya Mungu. Sauti ya Mungu hulijia Neno.

¹³⁸ Ndipo Ibrahim akaenda moja kwa moja kule juu kwenye ile Sauti, na tulivu, Sauti ndogo ya Mungu, kwenye Neno la Mungu, hana budi kuutoa uhai wa mwanawewe.

¹³⁹ Akasema, “Usimnyoshee mkono, Ibrahim. Ninajua unanipenda sasa. Na wale wote baada yako, haleluya, wale wote watakaokuja baada yako, walio tayari kulichukua Neno Langu, watakuwa ni Uzao wako, na hapo atamiliki mlango wa adui.”

¹⁴⁰ Laiti ningalikuwa na wakati wa kuwaambia jambo fulani lilitotukia siku chache zilizopita, unaona, juu ya yale yaliyotukia. Loo, jamani!

¹⁴¹ “Utamiliki mlango wa adui; uzao wako baada yako. Ibrahim, anayekubariki atabarikiwa, na anayekulaani atalaaniwa.” Yesu alisema, “Yafaa jiwe kubwa la kusagia lifungiwe shingoni mwako, na kutoswa katika kilindi cha bahari.”

¹⁴² Na madhehebu haya yanayowafukuza hao watu wacha Mungu, kwa sababu wanaiteetea Kweli, lile Neno, na Roho na nguvu za Mungu, na kudumu kwa Neno, mnaona kilichotukia? Wametoswa katika bahari ya usahaulifu.

¹⁴³ “Yafaa jiwe kubwa la kusagia lifungiwe shingoni mwako, na utoswe katika kilindi cha bahari, kuliko hata kumkosesha mmojawapo wa wadogo hawa Walioitiwa mafuta.” Hao ni akina nani? Uzao wa Ibrahim ukishikilia Neno la ahadi.

¹⁴⁴ Baadhi ya makanisa yetu yanafikia mahali wanapokana. Wanakana uponyaji wa Kiungu. Hawautaki kanisani mwao tena. Hiyo ni kweli. Madhehebu yetu ya Kipentekoste hawataki uponyaji wa Kiungu tena. Ni kitu gani? Hivi hamwonji jinsi ibilisi amefanya kazi? Ameenda kule na kusema mambo ya uongo namna hiyo. Na watu wenyewe akili tu wakiwazia kwamba wao ni wa kiroho, na kuangalia jambo hilo, na kusema, “Angalia *lile*. Angalia *lile*.” Mimi siangalii hilo.

¹⁴⁵ Kama wewe ni Uzao wa Ibrahimu, utaangalia ahadi ya Mungu, yale Mungu aliyosema yafanywe kulihusu. Jambo ndilo hilo. Uzao wa Ibrahimu, tunaangalia ahadi. Sijali ni wangapi wanaanguka *huku* na ni wangapi waanaanguka *kule*. Ahadi inadumu kweli.

¹⁴⁶ Inakupasa kupitia kwenye majaribio hayo. Unaona? Naam. Ibrahimu, kwanza alijaribiwa, halafu akatiwa muhuri, ndipo akapewa ahadi ya kwamba “Uzao wake unapaswa kumiliki mlango wa adui.” Ninapenda jambo hilo. Ndipo, walimiliki milango ya adui yao wakiisha kujaribiwa.

¹⁴⁷ Jambo ni kwamba, hatuwezi kustahimili majaribio. Hiyo ndiyo sababu madhehebu yetu hayawezi kustahimili majaribio. Si mapenzi ya Mungu. Ni, Mungu ameyabariki, bali si mapenzi ya Mungu. Kwa sababu, unaona, una kundi zima la watu hapa likiwa na mawazo chungu nzima, nao wanayakusanya pamoja na kutokea na mazuri kabisa wawezayo. Baadhi yao wanasesma, “*Huyu* ni mtu mkubwa. Huwezi kukataa neno lake.” Vema, hivyo ndivyo kanisa Katoliki liliivyounda dhehebu, jambo lile lile, juu ya kundi la waaminio wa kielimu. Wenyewe elimu, wanaliangalia, wanilibadili kuendana na nyakati. Huwezi kufanya hivyo. Kila kitu kingine ni uongo ila Neno la Mungu.

¹⁴⁸ Ibrahimu kamwe hakuangalia kitu kimoja ila ahadi ya Mungu. Haidhuru ilikuwaje, yeye alidumu na ahadi ya Mungu.

¹⁴⁹ Basi hiyo ndiyo sababu hatupati zaidi. Dhehebu haliwezi kumiliki lango la adui. Kuna nia nyingi mno potovu mle ndani.

¹⁵⁰ Inabidi kumchukua mtu binafsi, anayemiliki mlango wa adui. Unaweza kufanya hivyo kama ukitaka. Naam, bwana.

¹⁵¹ Hebu na tujaribu wachache, kwa dakika chache, tuone kama wanadumu katika Maandiko.

¹⁵² Sasa, kulikuwako na wakati huko Babeli wakati kulikuwako na sa—sanamu iliyowekwa, mfano mzuri wa kanisa Katoliki, na wote ambao hawakuisujidia sanamu hiyo wangechomwa kwenye tanuru ya moto uwakao. Sasa, lilikuwa ni shindano la kuamua, kama wangekaa, wakati Mungu aliyosema, “Msiwe na miungu wengine mbele Zangu, wala kufanya sanamu yoyote ya chochote.” Hivyo ndivyo Mungu alivyosema. Shindano la kuamua likaja.

¹⁵³ Israeli wengine wote walianguka moja kwa moja ndani. Na wakati baragumu ilipolia, na ninii—na zomari zikalia, na ninii—na filimbi zikalia, mbona, wote walisujudu mbele ya sanamu hii.

¹⁵⁴ Bali kulikuwa na watatu wao waliosema, “Hakuna kitu.” Walisikia Sauti hiyo ndogo tulivu, nao wakakaa sawa na Neno. Walifany nini? Walidumu na Neno.

¹⁵⁵ Na baadaye, wa—wa—walisema, “Msipofanya hivyo... Tutawapa nafasi nyingine, ama tutawatupa katika tanuru ya moto uwakao”

¹⁵⁶ Kasema, “Mungu wetu anaweza kutukomboa na tanuru hiyo ya moto uwakao.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “Lakini, hata hivyo, tutadumu na Neno.”

¹⁵⁷ Sasa, ndugu, na wewe je? “Nitafanya nini, Ndugu Branham?” Dumu na Neno. Dumu na ahadi. “Kanisa langu lote litaniacha.” Dumu na ahadi. Hayana budi kutoweke, yataondoka tu siku moja, kwa vyovyyote vile. Lakini, Mungu hataondoka. Dumu na ahadi. “Vema, nakuambia, watanifukuza.” Dumu na ahadi, vivyo hivyo tu. Wewe dumu moja kwa moja na ahadi. Sasa, kama unaweza kudumu na ahadi na kudumu pale, dumu moja kwa moja nao basi.

¹⁵⁸ Shiriki na kila mtu. Lakini sasa hapa, sasa, kamwe hutashinda kwa njia nyingine yoyote ila mbali na kushiriki na kila mtu. Inakupasa kufanya hivyo. Sasa, wakati walipoharibika sana, wao kwa utovu wa uadilifu, basi kaa mbali nalo. Hiyo ni kweli. Usiingie kwenye eneo la adui. Lakini mradi tu unajaribu kumvuta ndugu yako, hilo ni jambo lingine. Unaona?

¹⁵⁹ Sasa angalia. Lakini kamwe hutashinda maoni ya dhehebu, mtu mmoja. La, bwana. Wakati, wameweka sheria zao, “Tunaamini jambo *hili*, kituo kikuu!” Kama ukiandika fundisho lako, “Tunaamini jambo *hili*,” unaweka koma, ingekuwa ni tofauti. Kituo kikubwa kinamaanisha, “Tunaamini jambo *hili*, nawe huna budi kuja kwenye *hili* na kutia sahihi karatasi hii, la sivyo hakuna lingine.”

¹⁶⁰ Lakini kama ukisema, “Tunaamini jambo *hili*,” koma, “pamoja na kadiri tunayoweza kujifunza kutoka kwa Mungu. Sisi tuko wazi kwa Roho Mtakatifu,” basi unaendelea, ndugu. Naam. Hilo litakuwa tofauti sasa.

¹⁶¹ Lakini, unaona, kama umeliandika kwa kituo kikubwa, na Mungu atoe jambo fulani lingine litokee, lithibitike kwamba ni Neno Lake, ile Kweli, huwezi kusonga mbele, kwa sababu ni “kituo kikubwa.” Hicho kinalimalizia. Hapo ndipo Walutheri walipofia. Hapo ndipo Wamethodisti walipofia. Hapo ndipo Wabaptisti walipofia. Hapo ndipo Wapresbiteri walipofia. Na hapo ndipo Wapentekoste wanapofia. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Wanafia pale pale, hebu angalia, maana tayari li—

limeandikwa. Hakuna kitu u—unachowenza kuliongezea wala kulipunguza. Liko—liko hapo. Hilo ni fundisho lako.

¹⁶² Mlutheri asingekubali utakaso. La, bwana. Tayari alikuwa amesema, “Wenye haki wataishi kwa imani.” Si Martin Luther; bali hilo kundi lililomfuata. Hiyo ni kweli.

¹⁶³ Si John Wesley; bali lile kundi lililomfuata. Hiyo ni kweli.

Si Calvin; bali kundi lililomfuata.

¹⁶⁴ Si John Smith wa Kanisa la Kibaptisti, ambaye aliomba sana, wakati wa usiku, hata macho yake yakavimba yakafunga, kwa ajili ya kanisa lake; na mke wake hana budi kumwongoza na kumlisha pale kwa kijiko, mezani. Si yeye; bali kundi hili la Wabaptisti linalomfuata, shirika lililokuja nyuma yake.

Si Alexander Campbell; bali wale waliomfuata.

¹⁶⁵ Si uamsho wa kipentekoste hapo mwanzo, waliokuwa na vitu vyote shirika, na wakashirikiana na kila mtu; bali yale makundi yaliyokuja na kusema, “La. Sisi ni *hili*, na sisi ni *hili*. Na *hizi* ni hoja, na mambo kwisha kwisha!” (“Wakijitenga, yaonekana hawana Imani.”) Kweli. Hicho ndicho kilichosababisha jambo hilo. Hicho hapo kitu kiovu. Amina. Ninajisikia sawasawa, asubuhi ya leo.

¹⁶⁶ Wana wa Kiebrania, baada ya kustahimili jaribio, kama watadumu na Neno la ahadi, ama hawatadumu, walijaribiwa. Nao walifanya nini? Walimiliki mlango wa adui. Amina. Kwa nini? Walidumu kwenye Neno.

Dumu na Neno, hiyo Sauti ya Mungu inayonena nawe.

¹⁶⁷ Sasa, hoja zote zilisema, “Sasa, angalia. Babeli, haitakuwa tofauti hata kidogo. Kwa sababu, sisi, tunaposujudu mbele ya sanamu hii, tunamwabudu Mungu, kwa vyovoyote vile. Vema, kama tukifanya jambo hilo *hivi*, tunalimaanisha *hivi*.”

Lifanye jinsi Mungu alivyosema.

¹⁶⁸ Vipi kama Mungu alisema, “Musa, vua viatu vyako, Musa. Wewe uko mahali patakatifu.”

¹⁶⁹ Aseme, “Asante, Bwana. Hakika ninakuamini. Nitavua tu kofia yangu, badala yake. Ni udhia sana kufungua kiatu changu.” A-ha. Aha! Haingefanya kazi kamwe.

Yeye alisema, “Kiatu.” Hakusema “kofia.” Kweli.

¹⁷⁰ Inakubidi kuja, mstari kwa mstari, yale asemayo Mungu, na ujiweke sawa na Neno Lake.

¹⁷¹ Sasa, baada ya wao kujaribiwa, walimiliki mlango wa adui wa moto. Walikuta kwamba, walipokwenda moja kwa moja hata mwisho, wakidumu kwenye Neno la Mungu, waliumiliki mlango huo. Hiyo ni kweli. Baada . . .

¹⁷² Danieli. Kulikuwako na tangazo lililotolewa, na kutiwa sahihi na Waamedi-Waajemi, ambalo lisingeweza kubadilishwa,

ya kwamba, "Kama mtu yejote akimwomba mungu mwengine yejote, na atupwe kwenye tundu la simba." Naye Danieli alijua ya kwamba Neno la Mungu lilikuwa, kumwomba dua Yeye peke yake, kwa hiyo alifungua tu madirisha na kuomba kwa vyovyote vile. Sasa, hakurudi pembeni. Alifungua madirisha kuelekea hekaluni. Hakulionea haya jambo hilo.

¹⁷³ Nasi hatutaki kutekeleza dini yetu Jumapili, na Jumatatu tufanye jambo lingine. Ama, tuamini moyoni mwetu jambo moja, tuje mbele ya mtu mwengine na kusema, "Vema, sijui. Naam, nafikiri unasema kweli." Kuwa kile ulicho. Kama huko sawa, ondoka mimbarani, ondoka kanisani. Hiyo ni kweli. Maana, wewe ni kikwazo kwa vyote viwili. Kaa jinsi ulivyo. Sema unachoamini, ndipo huna kitu cha kughairi. Unasimamia ukweli hasa. Kila mtu anajua tabia zako. Wanaume watakuthamini, mwanamume yejote.

¹⁷⁴ Mwanamke anaweza kuwa na sura mbaya kupindukia. Huenda akawa ni mkubwa, mnene, mdogo, amekonda sana, mwenye nywele nyeusi, macho ya hudhurungi, macho ya bluu, macho ya kijivu; mmoja, njia moja, na mwengine nyingine. Lakini kama mwanamke huyo ni safi, mama wa heshima, hakuna mwanamume nchini ila yule angaliawulia kofia yake, kama ana wakia moja ya mwanamume ndani yake. Kweli. Kwa sababu, yejote—yejote anatoa kile alicho, na wanaume wanathamini jambo hilo.

¹⁷⁵ Vivyo hivyo Mungu atamthamini mwanamume ambaye atakuwa kile alicho, ama wanaume wanaokiri Ukristo. Hebu na tuwe Mkristo, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, akiwa na Neno la Mungu, vinginevyo tusahau jambo hilo. Kweli. Maana, vinginevyo, unakuwa unafiki, na kuishi maisha tofauti. Na watu wanakuona unakimbia huku nje kwenye dansi, na kuvuta sigara, na mambo kama hayo, na ukidai kuwa Mkristo, basi, unaona, unaweka jiwe la kujikwaa katika njia ya wengine.

¹⁷⁶ Mnaona ninyi wanawake, wakati mwengine, jinsi wanavyokata nywele zao na kuvaan na kutenda katika nguo hizi fupi chafu, wanaonekana kama mnyama aliyechunwa ngozi ama chochote kile, na akienda huko mitaani, akitembea huku na huko, visigino virefu *hivi*, wakitembea kwa hatua za madaha barabarani. Je! hiyo ni ya kipentekoste? Ndipo ma—makanisa mengine yanasema, "Wanadai wana kitu ambacho hawana."

¹⁷⁷ Umetiwa muhuri na kutiwa alama na Roho Mtakatifu. Huko kwenye ukumbi wa dansi usiku wa leo na kukumbatiwa katika mikono ya mwanamume fulani, ambaye siye mume wako; kesho yake usiku, kisha unarudi kanisani na kucheza dansi kila mahali. Hiyo si pentekoste. Huo ni unafiki. Huo ni uchafu.

¹⁷⁸ Zaidi sana siwaambii ninyi. Lakini, mnatambua, kanda hizi zinazotengenezwa hapa husambazwa kote ulimwenguni, kwa hiyo ninahubiri tu kana kwamba ni kwa ulimwengu mzima.

Ninapomhisi Mungu akisema, "Sema jambo fulani," ninalisema tu, kwa kuwa sijui linakoenda. Hiyo ni juu Yake kushughulikia jambo hilo. Dumu tu na Neno. Hiyo ni kweli. Vema.

¹⁷⁹ La, Danieli asingesujudu tangazo lao, kama alitupwa njie ya dhehebu hilo ama hakutupwa. Yeye alikaa moja kwa moja dirishani, naye akadumu na Neno la Mungu. Hakulionea aibu.

¹⁸⁰ Kulitukia nini? Walimtupa kwenye tundu la simba, bali yeye alimiliki mlango ya tundu la simba. Kwa nini? Utukufu! Kwa sababu Mungu alisema ninii yake... "Uzao wako utamiliiki mlango wa adui." Hata adui awe ni nini, unamiliki mlango huo. Loo, ni mara ngapi ambapo tungeweza kuninii...?

¹⁸¹ Mwangalie Musa, akifuata njia ya amri za Mungu, alishuka akaenda Misri, ilionekana kana kwamba kila kitu kilikuwa kiko kinyume. Alikuwa na waigaji fulani walioambatana naye. Alishuka akaenda na baadhi ya i-ishara, kuonyesha ya kwamba alikuwa ametumwa. Akatupa chini nyoka, na kadhalika namna hiyo.

¹⁸² Na hawa hapa waigaji wakaja, wakatupa zao chini. Yeye angeweza kufanya nini? Hakuna kitu. Mungu hakumwambia watafanya hivyo. Alitaka kumjaribu Musa. Yeye ndiye aliyewaruhusu Yane na Yambre kutupa nyoka zao chini, ama fimbo zao.

¹⁸³ Kwa hiyo hapo alisimama Musa kwenye wajibu wake. Akatupa fimbo yake chini. Ikageuka ikawa nyoka. Akasema, "Angalia jambo hilo, Farao. Hivyo ndivyo Bwana wangu alivyoniambia nije, nifanye mbele zako."

¹⁸⁴ Farao akasema, "Njoni hapa, Yambre na Yane." Wakatupa fimbo zao chini. Zikageuka zikawa nyoka, vile Musa alivyofanya.

¹⁸⁵ Hivi uso wake ulikuwa Mwekundu? La, bwana. Angali aliamini Mungu alimtuma. Alidumu na ahadi hiyo. Na ni jambo gani lililotukia?

¹⁸⁶ Hapo ndipo wakati unapokuwa mbele ya baadhi ya mikutano yako ya mahojiano. Huenda uso wako ukawa mwekundu, kidogo. Dumu na Neno.

¹⁸⁷ Ni kitu gani kilichotukia? Mara, swila huyu mkubwa wa Musa alikuja akawameza. Mungu alithibitisha. Baada ya jaribio lake, yeye alisema, "Ninakutaka, kwa ishara hii, uwaache wana hao watoke waende kule. Ninataka uwaturidishe nyumbani, makwao. Mungu alishuka hapa chini kusema, alinituma huku kuwakomboa. Ninataka warudi." Yeye alitupa hiyo pale chini.

¹⁸⁸ Loo, jaribio likaja. Musa, utafanya nini, utageuka, uende zako, useme, "Vema, huenda nilikuwa nimekosea"? La, bwana.

Musa alisimama pale pale, "Mungu aliagiza jambo hili." Utukufu!

¹⁸⁹ Mungu akisema jambo lolote, dumu Nalo. Haidhuru ni jambo gani linalotukia, dumu Nalo. Wakikufukuza na kusema, “Hatutashirikiana, hatutafanya *hili*,” dumu Nalo.

¹⁹⁰ Musa alidumu moja kwa moja nalo. Ni jambo gani lililotukia? Alimiliki mlango wa adui yake. Haleluya. Ibilisi akasema, “Nitaitandaza Bahari ya Chumvi mbele yako,” lakini ilifunguka. Wasingeweza kuwaweka Misri tena. Alimiliki mlango wa adui. Kwa nini? Kwa sababu alidumu na agizo alilopewa na Mungu. Amri za Mungu, yeye alidumu na Neno la Mungu na ndipo akamiliki malango ya adui.

¹⁹¹ Yoshua, baada ya kupitia kweneye jaribio. Alikuwa huko chini, labda, na akaogelea kuvuka Yordani, yeye na Kalebu, pamoja na wale wapelelezi. Aliporudi kutoka Yordani, walifika Kadeshi-Barnea. Na hao wote wakasema, “Loo, kama tukianza, hilo litavunja madhehebu yetu vipandevipande. Kamwe hatuwezi kuinga.”

¹⁹² Roho hiyo haifi. “Loo, hatuwezi kuchukua jambo Hilo. Kama tukifundisha watu wetu jambo Hilo, tutafanya nini? Tutatoa karibu nusu ya mashemasi, kanisani, nje. Wameoa mara mbili, mara tatu. Tutafanya nini? Sisi, loo, kama tukiwaambia wanawake wetu ya kwamba inawabidi kuwa na nywele ndefu, unajua wangefanya nini? Wangeondoka kanisani. Nasi tungefanya nini? Loo, tungehesabiwa tu kuwa wa mtindo wa kale.” Yesu alikuwa wa mtindo wa kale, pia. “Hatuwezi kufanya hivyo. Hatuwezi kufanya hivyo. Imetuzidi.”

¹⁹³ Unajua pale mwaminio mkwamia mpakani anapofikia. Waebrania, mlango wa 6, inaelezea jambo hilo. “Yeye aliyekwisha kupewa nuru, waliofanywa washiriki wa Roho Mtakatifu, wakaanguka, kujifanya upya tena.” Alifika hapo mpakani na akakataa kuvuka, hivyo tu, akakataa kuamini kabisa.

¹⁹⁴ Maana, Kalebu alifanya nini? Yoshua alifanya nini? Yeye alisema, “Sisi tunaweza hata na zaidi kuiteka.” Kwa nini? Wao walidumu na yale Mungu aliyoahidi.

¹⁹⁵ Loo, wao walisema, hao wengine walisema, “Vema, hao ni majitu. Wamejizungushia kuta kabisa. Wako *hivi*. Mbona, tusingeweza kuwagusa, kwa njia yoyote.”

¹⁹⁶ Yoshua akasema, “Tunaweza hata na zaidi kufanya jambo hilo. Tulieni, enyi watu! Nyamazeni! Ketini chini!” Amina.

¹⁹⁷ Ninawaambia, imani iko katika jambo kubwa mno, inapokuja juu ya Neno la Mungu. Yeye haogopi basi. Imani ina nywele kifuani, misuli mikubwa. Inasema, “Nyamazeni!” Kila kitu kinginecho kinakimbilia pembeni, hiyo ni kweli, Mungu anaponena. “Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakae ndani yenu, semenii mtakalo.” Haya basi. Loo, ninapenda jambo hilo. A—ha!

Pepo watatetemeka, wenyе dhambi wataamka;
Imani katika Yehova itatikisa kitu chochote.

¹⁹⁸ Unawezaje kuwa na imani wakati unapojuia hufanyi kazi, hutembeи katika Neno Lake, wakati unapojuia kuna mambo pale unayopaswa kusema wala huyasemi? Kuna mambo pale unayopaswa kufundisha wala huyafundishi. Kuna mambo pale usiyoweza kusema, na unawezaje kuwa na imani wakati ukijua umekosea?

¹⁹⁹ “Kama miyo yetu isipotuhukumu.” Haya basi. Haya basi. Bali dumu na Neno hilo, ambamo hakuna kitu kilichohukumiwa. “Hakuna hukumu ya adhabu juu ya walio katika Kristo Yesu, wanaoenenda si kwa mwili bali kwa Roho.” Roho huongoza kwa Neno, maana Roho anawenza kutoka tu kwenye Neno, maana Neno Lake ni Roho. Nalo linaweza tu . . . Roho halisi na wa kweli wa Mungu anawenza tu kunena Neno la Mungu. Loo, jamani! Jamani, jamani!

Nenda zako, ulimwengu. Shetani, tuache.

²⁰⁰ Usiogope kuuambia mlima huu, “Ng’oka.” Nena hilo. Kaa pale, uangalie ukiporomoka. Hiyo ni kweli.

²⁰¹ Bali ukiwa na kuhukumiwa kokote pale, afadhali—afadhali utulie. Unaropokwa tu basi. Husemi kweli. Huneni mambo unayopaswa kunena. Vema.

²⁰² Tunaona ya kwamba basi Yoshua, baada ya kupitia kwenye jaribio hilo, aliona ushahidi wa nchi nzuri, naye akasimama pale Kadeshi-Barnea na kuwalalamikia wote, na kusema, “Sisi tunaweza hata na zaidi kuiteka. Tunaweza kuiteka.” Wazo lilikuwa ni kitu gani? Kuvuka.

²⁰³ Wazo la Musa lilikuwa ni nini? “Onyesha ishara hii na uwatoe wana.” Na lilionekana kana kwamba lilihindwa. Bali ye ye alidumu na Neno, nao mlango wa Bahari ya Chumvi usingeweza kumzuia. Aliipitia hiyo moja kwa moja. Alimiliki mlango wa adui.

²⁰⁴ Yoshua, akiangalia ahadi ya Mungu, alisema, “Sisi tunaweza hata na zaidi kuiteka.” Hiyo ni kweli. Na wakati alipofika pale Yordani, ulifanya nini? Ulifungua njia. Amina. Jambo ndilo hilo. Alimiliki mlango wa adui. Hiyo Yordani ilikuwa ikimzuzia kuvuka na kuitwaa ile ahadi. Bali wakati alipofika kule chini, ye ye alikuwa ni Uzao wa Ibrahim. Kwa nini? Aliamini Neno la Mungu. Hivyo ndivyo tu unavyoweza kuwa Uzao wa Ibrahim, ni kuamini Neno la Mungu. Na halafu basi ye ye alifanya nini aliposhuka akaja mahali alipokuwa tayari kukabiliana na adui? Mungu alifungua mlango, naye akaumiliki, akautwaa, akavuka.

²⁰⁵ Wakati vita vya kwanza, mapambano yake ya kwanza aliyopambana nao, kuta hizo zilikuwa kubwa sana wangeweza kushindana mashindano ya magari juu ya hizo. Ataingajie

awapate? Walimtoroka, wakarudi ndani. Adui atafanya hivyo, pia. "Bali utamiliiki mlango wa adui."

²⁰⁶ Kasema, "Bwana, yanipasa nifanye nini?" Alizunguka, alasiri moja, akitafakari. Alimwona Mwanamume amesimama amechomoa upanga wake. Yoshua akauchomoa upanga Wake, kasema, "Je! wewe u upande wetu? Wewe ni wa adui zetu?"

Akasema, "Mimi ni Amiri wa jeshi hili."

"Yanipasa nifanye nini?"

²⁰⁷ "Uzunguke, mara kumi na tatu. Piga baragumu. Utaumiliiki mlango wa adui."

²⁰⁸ Ulianguka chini. Naam, bwana. Kwa nini? Yeye alikuwa ni Uzao wa Ibrahimu, aliyelishika Neno la Mungu. Yeye alimiliiki kila mlango uliomjia. Hakika.

Muda umeenda sana. Yanibidi kuondoka.

²⁰⁹ Angalia, mashujaa hawa wote wa thamani, nina ukurasa mzima uliojaa wao walioandikwa hapa chini. Lakini mashujaa hawa wote wa thamani, mambo waliyofanya, hatimaye walikuifa.

²¹⁰ Lakini baadaye ukaja ule Uzao halisi wa imani, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, Yesu, ahadi. Ibrahimu alimzaa Isaka, kweli, kwa jinsi ya mwili, bali ule Uzao halisi haukuwa katika mfumo huo wa dhehebu. Ulikuwa katika ile ahadi ya Neno la Mungu, ya kwamba angemfanya baba wa mataifa, si kupitia kwa Isaka, bali kupitia Uzao wa Kifalme, Yesu. Huo ndio uliokuwa Uzao wa Kifalme, ambao, kwa kweli, Uzao wa Ibrahimu. Yesu hakuwa Myahudi, wala hakuwa Mmataifa. Yeye alikuwa ni Mungu. Unaona? Ninii...

²¹¹ Ninyi Wakatoliki hapa, nawatakia heri. Lakini mnapomwabudu Mariamu kama mungu mke, mna shida gani, kwa vyovyyote vile? Mariamu hakuwa kitu ila mwanamke. Mungu alimchagua. Yeye alikuwa ni kiangulio. Hivyo tu. Kiangulio, hivyo ndivyo mwanamke alivyo, bali anahuksika na mbegu ya mwanamume.

²¹² Lakini, ni kusanyiko lililochanganyikana, bali sina budi kusema jambo hili kusudi mpate kufahamu ninalozungumzia. Sasa, ninyi humsikiliza da—daktari wenu, na mimi ni ndugu yenu. Hakika, mnaweza.

²¹³ Mariamu hakuwa na chavua katika Kristo. Hakukuwako na hisia za jinsia wakati Roho Mtakatifu alipomtia uvuli, hata kidogo. Lakini Mwenyezi Mungu, Muumba, aliumba seli ya Damu na chavua. A-ha! Kama ilikuwa ni chavua kutoka kwa Mariamu, basi wafu hawafufuki.

Utukufu! Hilo limekuja tu jipyga. Nimelipata hilo sasa hivi.

²¹⁴ Basi kama ukisema hakuna tofauti, yale tunayofanya, basi ni kwa nini Mungu akatwambia tuachane na mambo mabaya?

Kwa nini Mungu aliufufua mwili wa Yesu, kama sivyo ilivyo? Kwa hiyo, unaona, kusingekuwako na mwanamke aliyehusika katika jambo hilo. Kama alikuwako, basi mwili Wake ultokana na mama Yake, Mariamu, kwa sababu alifanya tendo la jinsia kwa kutiwa uvuli na roho ambaye alimfanya ku—kutoa shahawa, na ni kosa. Roho Mtakatifu, kwa kuzaliwa bila dhambi, haleluya, hapo aliumba shahawa za mwanamume na za mwanamke pia.

²¹⁵ Je! Yesu alimwita “mama”? Chunguza hilo katika Maandiko. Yeye alimwita “mwanamke” Haleluya! Mwanamke! (Hilo ni jipya. Hiyo ndiyo sababu linatendeka jinsi linavyotendeka.) “Mwanamke, mtazame mwanaao.” Karibu naye maili milioni moja kuliko Yeye alivyo kuwa.

²¹⁶ Yeye alikuwa Mungu. Yeye hakuwa Myahudi wala Mmataifa. Yeye alikuwa Mungu, nyama na mwili pia, Mungu akiishi ndani Yake. Ati Mungu akiishi katika shahawa ya mwanamke? Isingewezekana. Shahawa hiyo ya mwanamke ilibidi iwe na uhusiano fulani na miili yetu. Bali ilikuwa ni Damu pamoja na shahawa, ambazo Mungu alizitia uvuli.

²¹⁷ Yeye angeweza kuiweka juu ya kisiki kama angetaka. Naam, bwana. Yeye angeweza kuiweka popote alipotaka.

²¹⁸ Lakini aliileta kwa sababu mwanamke alikuwa katika lile anguko. Hapo alitokea Mwana asiyé na dhambi wa Mungu aliye hai, aliyeumbwa, akazaliwa na bikira, mwili na nafsi pia.

²¹⁹ Kwa nini Daudi akasema, “Sitamwona Mtakatifu Wangu... sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu, Mtakatifu Wangu aone uharibifu. Wala sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu”? Daudi alisema hivyo. Unaona? Vyote nafsi, mwili, na roho pia, ziliumbwaa na Mungu, kwa Yeye.

²²⁰ Mwanamke huyo hakuwa mama. Alikuwa mwanamke. Ninaamini alikuwa ni mwanamke mwaminifu, mtakatifu. Kweli kabisa. Kamwe hakuwa amekuwa kiangulio. Mungu kamwe asingechagua kiangulio kichafu. Bwana akipenda, ninahubiri juu ya jambo hilo usiku wa leo, lakini, “Maskini kiangulio kichafu ni nini?” Kumleta nanii Wake, kumleta Mwanawee duniani katika hicho, Yeye alimchagua “bikira asiyemjua mwanamume yeyote.” Wala hakutoa shahawa yoyote wala chochote kile wakati Roho Mtakatifu alipomtia uvuli. Kwa sababu, Mungu, katika njia yake safi sana, isiyo na kikomo, aliumba ndani yake: nafsi, mwili, na roho, ya Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Yeye alikuwa Mwana wa Mungu aliyezaliwa na bikira.

²²¹ Hilo lilifanya nini? Livilunja mlango wa adui. Haleluya! Whiu! Hili linakuwa zuri, kwangu. Angalieni. Kwa nini? Yeye alivunja mlango wa adui papo hapo, ili kwamba kila mtu aliyezaliwa katika ulimwengu huu kwa tamaa ya kujuana kimwili, ambaye asingeweza kwenda Mbinguni kwa sababu kujuana kimwili ndiko kulikoanzisha jambo hilo hapo mwanzo, katika bustani ya Edeni, ndiyo sababu walijifunika. Alipofanya

jambo hilo, alivunja kitu hicho vipande viwili papo hapo, na kumiliki mlango wa adui. Kwa kitu gani? Kuchukua Uzao wa kifalme wa Ibrahim, kwa mara ya kwanza kabisa, na kukivunjilia mbali kabisa. Uzao wa Kifalme wa imani na ahadi, sio kuzaliwa na Mariamu, bali na Mungu, kulivunja milango. Hiyo ni kusema, huwaachilia wanadamu wapitie mlangoni. Utukufu kwa Mungu!

²²² Yeye alifanya nini? Ndipo alichukua milango yote ya adui. Aliuchukua mlango wa magonjwa. Magonjwa yasingeishi Mbele Zake. La, bwana. Wala hakuna kitu kingine kingaliishi Mbele Zake. Msafara wa mazishi usingeweza kusimama Mbele Zake. La. Yeye alifanya nini?

²²³ Yoshua alikufa. Musa alikufa. Hao wengine wote walikufa, bali si Uzao huu wa Kifalme. Mauti yasingeweza kusimama mahali Uzima ulipokuwa.

²²⁴ Yule mwanamke kutoka Naini, akitoka pamoja na mvulana wake. Alisimama na kusema, "Simama, mwanangu."

²²⁵ Yule msichana aliyekuwa amekufa, binti wa Yairo, Yeye alisema Neno huko nyuma katika ulimwengu usiojulikana huko nje, na kusema, "Binti, simama."

²²⁶ Lazaro, aliyekuwa amekufa kwa muda wa siku nne na mwili wake ukaiza, na nafsi yake ilikuwa imeutoka, kwa muda wa siku nne. Yeye alisema, "Lazaro, njoo huku." Utukufu!

²²⁷ Huyo hapo. Yeye alifanya nini? Alivunja mihuri ya kila kitu. Haleluya!

²²⁸ Wakati ilipombidi kufa basi, Yeye asingeweza kuushikilia uhai ule. Asinge kufa kamwe, bali ilimpasa kuutoa uhai huo. Na hapo alipoutoa uhai huo, Yeye alikufa mauti. Na nafsi Yake ya thamani, kama vile Biblia ilivyosema, ilishuka katika kuzimu, kupachukua mahali pangu na mahali pako. Uzao wa Kifalme wa Ibrahim! Nini? Yeye alikuwa ni ule Uzao wa Kifalme. Loo, utukufu!

²²⁹ Sasa sisi ni Uzao wa Kifalme, wale, ambao hudumu na Neno, kama jinsi Yeye aliviyokuwa hasa. "Kwa maana hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu; Naye Neno, alifanyika mwili, akakaa kwetu." Hivi huoni mahali Uzao huo wa Kifalme ulipo? Uzao wa Kifalme ni ule unaodumu na Neno.

²³⁰ Enyi dhaifu mlion tayari kapatana na ibilisi, na mitindo yake ya ulimwengu. (Siwazungumzii ninyi hapa.) Huko nje, ninyi wahubiri mnaojua ya kwamba mnahubiri siku za miujiza zimepita, mnahubiri ya kwamba hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu, mnatia aibu, na mnajiita Uzao wa Ibrahimu.

²³¹ Uzao wa Kifalme hudumu na Neno. Uzao wa Kifalme, usiozaliwa na mwanadamu, hauna uhusiano wowote na mwanamume wala mwanamke. Mwanamke ni kanisa; hauna

uhusiano wowote na kanisa. Mariamu hakuwa na uhusiano wowote na ule Uzao. Wala kanisa, linaloijiita dhahebu, halina uhusiano wowote na ule Uzao. Umezaliwa na kitu gani? Si na dhehebu, si na Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Katoliki, Lutheri, na kadhalkika.

²³² Bali, umezaliwa na Uzao wa Kifalme wa ahadi ya Mungu, huo ndio unaoteka mlango wa adui. Tayari umetekwa kwa ajili yake. “Kwa maana mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo, mtatendewa.” Haya basi. Ni ahadi. Tayari imetimizwa.

²³³ Nafsi Yake ya thamani ilishuka ikaingia kuzimu, ambako nilipaswa kwenda. Lakini katika siku hiyo ya tatu . . . Samsoni akiubeba mlango wa mji mgongoni mwake, hakuwa na uhusiano wowote nao. Yeye alichukua milango ya kuzimu, milango ya kaburi, na kila kitu kinginecho. Hakuubeba mlimani, bali aliuangamiza. Haleluya! Alimiliki mlango wa adui.

²³⁴ Angahewa zilizojaa nguvu za ibilisi, huko juu, ambapo Malaika wala chochote kile kisingeweza kushuka. Kusingekuwako na kuombewa dua kokote, kwa maana damu ya mbuzi isingeweza kuondoa dhambi. Bali Damu Yake mwenyewe iliondoa dhambi.

²³⁵ Naye alipaa Juu, akateka mateka. Aliwapa wanadamu vipawa. Sasa, kila mmoja wa Uzao wa Ibrahimu anayetaka kulipia gharama, kushuka na kutubu dhambi zao, kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zako, kujazwa tena na Roho Mtakatifu, na kustahimili majaribio.

²³⁶ Nao wanapouondo ulimwengu ndani yako, mambo ambayo yameondoka, kila kitu ambacho ni kibaya, kila kitu kinachoonekana kuwa ni kibaya, kama vile wanawake na nywele zao, wanaume na matendo yao mabaya, na makanisa na madhehebu yao, na nanii—mchungaji atakayetawaliwa na mashemasi wake, na—na mambo yote ya aina hiyo. Kundi fulani la kilimwengu la chochote kile linaingia mle na kumfanya maskini mchungaji, kumfukuza kanisani.

²³⁷ Endelea, mchungaji. Mungu akubariki. Dumu na Neno. Usichukue chochote.

²³⁸ Alipaa Juu. Alifanya nini? Alikata tundu, mlango, ambaao, maombi ya Uzao huu wa Ibrahimu. Kwa nini? Kwa nini? Kama sisi ni Mwili wa Kristo, kama tumekufa, tunajihesabu tumekufa na kuzikwa katika Kristo, na kufufuka pamoja Naye katika ufufuo. Yeye ndiye Kichwa cha Mwili. Palipo na Kichwa, Mwili upo pamoja Nacho. Halafu basi, asubuhi ya leo, ambapo kila mtu ambaye amefanya jambo hilo, “ameketi pamoja Naye katika ulimwengu wa roho,” pamoja na Uzao wa Kifalme. Mungu asifiwe.

²³⁹ Hakuna milango. Huwezi kuomba umbali *huu*, na kusema, “Loo, loo, hilo *hapo* neno.” A-ha. Wanakufungia nje, papo *hapo*.

²⁴⁰ Lakini mioyo yetu isipotuhukumu; kama tunajua ya kwamba tunatembea katika amri za Mungu; tunaona maisha yetu yamesafishwa; tunaona jambo hilo; kila Neno ambalo Mungu aliahidi, tunalitimiza; basi milango ya kila adui imemilikiwa. “Basi ombeni mtakalo, nanyi mtatendewa.” “Atamiliki mlango wa adui *yake*.” Loo, ndugu, hilo lingekuwa ni kanisa la jinsi gani!

²⁴¹ Nitakaporudi tena Phoenix, Bwana akiniruhusu, natumaini, nitakapoingia katika maskani hii, kwamba benchi hizi zitajazwa, na kila benchi katika shirika la full Gospel humu mjini itajazwa na watakatifu wa Mungu aliye hai: wanaoonekana kama Wakristo; wanaozungumza kama Wakristo; wanaotenda kama Wakristo; huku Roho wa Mungu akitenda kazi mionganoni mwao, ambapo, kama mtu angetenda dhambi, Roho Mtakatifu angeitamka papo *hapo*.

²⁴² Ataitamka. Mmeliona kwenye mstari wa maombi, kama hapa juu madhababuni. Ambapo, anasema, “Wewe rudi kule na usahihishe hilo na mume wako. Nenda, ukamwambie mke wako ya kwamba ulikuwa umetoka, majuzi usiku, na mwanamke huyo, anayeketi mahali *fulani-fulani*.” Kama atafanya hivyo hapa, kwa kutembea katika Neno, nikisikiliza ile Sauti ndogo tulivu, atafanya hivyo ndani yenu. Ninyi ni Uzao wa Ibrahimu. Basi, hakuna dhambi.

²⁴³ Mhubiri, hivi usingependa kuona jambo hilo kanisani mwako? Uingie katika kanisa hili, na kuangalia mahali pote *hapa*, uwaone wanaume na wanawake pia, wacha Mungu, watakatifu, wameketi pale wamejaa nguvu za Mungu. Dhambi isingeweza kuingia. Mtu anaingia na kuketi, Roho anainuka na kusema, “John Jones, umetoka mahali *fulani*, mji, mahali *fulani-fulani*. Yupo hapa kutafuta kuponywa kwa mwili wake. Unaona? Yeye alifanya jambo *fulani* mahali *fulani*. Alifanya *hivi*. Inambidi kurudisha *hiki*, na kusahihisha jambo *hili*, ndipo Mungu atamponya kansa hiyo. BWANA ASEMA HIVI.” Jamani, jamani!

²⁴⁴ Nipe kanisa moja, nipe watu kumi, ambao, lulu halisi za Mungu, Uzao wa Kifalme, waweke watu hao pamoja, na uangalie litakalotukia. Nipe nyumba hii iliyojaa watu wa namna hiyo, nami nitakuonyesha Nuru ambayo ulimwengu utaikimbilia. Hiyo ni kweli. Hilo ndilo Mungu analotutaka tuwe. “Ninyi ni mji ulio mlimani.” Ninyi ni Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu. “Utamiliki mlango wa adui wake.”

²⁴⁵ Magonjwa, kuna sababu ya magonjwa. Kuna kisa cha mambo haya. Naye Mungu, Roho Mtakatifu, yupo hapa kufunua jambo hilo na kukwambia ni kwa nini hulipati jambo hilo.

Tuna shida gani? Haitupasi kushangaa, “Je! atafanya hivyo.” Anafanya hivyo tayari. Unaafanya nini?

²⁴⁶ Mwangalie nabii huyo. Yeye hakusikiliza upepo ukienda kasi, “Utukufu kwa Mungu! Haleluya!”

²⁴⁷ Hilo ni zuri. Sasa, kumbuka, sihukumu jambo hilo. Ninatumaini kila mtu anaelewa na jambo hilo. Mtu fulani alisema, “Ndugu Branham haamini katika kusema, ‘Utukufu kwa Mungu! Haleluya!’” Vema, niangaliensi hapa juu sasa. Ninaamini katika kupaza sauti, kunena kwa lugha, kucheza katika Roho.

²⁴⁸ Lakini, ndugu, unaposhindwa kusikia hiyo Sauti ndogo tulivu ya Neno, hicho ndicho kitu kinachokupata. Kitu ndicho hicho.

²⁴⁹ Eliya alijua uamsho huu wote ulikuwa ukiendelea huko nje. Lakini ye ye aliwa... Kamwe haukumvutia huko nje kwenye kitu hicho. Lakini wakati aliposikia ile Sauti ndogo tulivu ya Mungu, basi alivutiwa. Ndipo akaufunika uso wake, akatoka. Kwa nini? Eliya aliwa ni Uzao wa Ibrahim, akiwa analifuata Neno.

²⁵⁰ “Mkikaa ndani Yangu na Maneno Yangu yakae ndani yenu, basi ombeni mtakalo, nanyi mtatendewa.”

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja kwa maombi.

²⁵¹ Loo, enyi kanisa, vipi, ninapomaliza kuhubiri namna hiyo, jinsi ninavyojisikia! Roho ananiondokea, nami ninaangalia nyuma. Ninawaona watu ambao kweli wangeingia mfukoni mwao na kutoa chakula kutoka kwa watoto wao, wanipe mimi. Ninaona maskini wanawake hapa, labda wakiwa na nywele fupi. Wangefanya nini? Wangefanya lolote lile ulimwenguni kwa ajili yangu, wavezalo. Mwanamume anayeishi na mke kama huyo, na mimi ninamkatakata tu vipande, kwa hilo Neno, ninamuudhi, dhamira yake inashushwa chini. Na hata hivyo mtu huyo angetoka aende hapa nje na kufanya kazi nyingi sana, na kunitumia fungu lake la kumi. Kabisa. Hilo linanifanya nijisikie, unaona, ninarudi mwilini basi, unaona, hivi, hivi nilisema nini? Simaanishi kudhuru. Si hilo.

²⁵² Lakini, loo, ndugu, na mpenzi wangu maskini dada na ndugu, kama hilo ni Neno la Mungu, na huyu akiwa ni Roho Wake anayelifanya Neno hilo liwe hai, kwenu, itakuwaje katika Siku ya Hukumu? Ninajaribu kuwafanya tayari kwa ajili ya siku hiyo. Tafadhalini, tafadhalini lichukueni tu Neno Lake. Kama kamwe nikihubiri lolote ambalo si Neno, ahadi ya Mungu, basi mna haki ya kuja kwangu. Bali hilo ni Neno. Na ni kwa sababu ninawapenda.

²⁵³ Si kwa sababu si—siwataki kwenye mtumbwi. Ni kwa sababu mtumbwi huo hautawavusha. Mtaangamia, moja ya siku hizi.

²⁵⁴ Inawabidi kuja Hukumuni. “Aliye na hatia ya jambo dogo mno ana hatia ya lote.” Na unapojuja jambo lolote ni sawa kwako kufanya, ni Neno la Mungu na ahadi ya kulifanya, halafu hulifanyi, basi vipi kuhusu jambo hilo? Utaombwa kutoa sababu, vipi basi? Wakati Ujumbe huu asubuhi ya leo utakapokukabili huko ng’ambo kwenye skrini, kwenye Siku ya Hukumu, vipi kulihusu? Wazieni jambo hilo, marafiki. Huenda ukafa kabla siku haijaisha. Sisi sote huenda tukafa. Na jambo moja la hakika, mtakufa.

²⁵⁵ Nilisimama hivi majuzi nikmwangalia mama yangu, mimi nikiwa nimemshika mkononi mwangu. Nilimshika baba yangu muda mfupi kabla ya hapo, na kumwangalia akiaga dunia.

²⁵⁶ Nimewaona wakifikia mwisho wa safari, ambao walidhani wao kweli ni sawa. Waseme, “Loo, Ndugu Branham, loo, laiti ningalishi muda kidogo tu zaidi!” Wamekwisha chelewa sana wakati huo. Pia kumbukeni, mauti hayabadilishi nafsi. Hubadilisha tu mahali pake pa kuishi. Na kama ukiona jambo hilo, jambo fulani ndani yako. Uwe na busara sasa. Kama ukiona jambo hilo, kitu fulani ndani yako kikikufanya utende hivyo na kujisikia hivyo, jinsi ambavyo upaswi kujisikia, tubu asubuhi ya leo, je! utatubu, ewe rafiki? Njoo. Kuwa... Haikupasi kuwa hivyo. Wewe ni mtu mwenye mashaka. Ishi maisha ya kweli ya Uzao wa Kifalme. Mungu anakutaka leo.

²⁵⁷ Hivi waweza kuinua mkono wako, huku kichwa chako kimeinamishwa, na moyo. Useme, “Ndugu Branham, ninamwinulia Mungu mkono wangu. Kwa uaminifu, kutoka moyoni mwangu, hivyo ndivyo ninavyotaka kuwa. Kweli hivyo ndivyo ninavyotaka kuwa. Ni—nimevurugwa huku niliko na kila kitu kinginecho, lakini kweli si—sitaki kuwa hivyo. Ninataka kuwa vile ulivyokuwa ukizungumza asubuhi ya leo. Niombee, Ndugu Branham. Ninamwinulia Mungu mikono yangu, si kwako, Ndugu Branham, bali Mungu. Na moyoni mwangu, Yeye anaujua moyo wangu. Ninatamani kuwa namna ya Mkristo unayenena habari zake, Uzao wa kifalme wa Ibrahim, kwa njia ya Yesu Kristo.” Inua mkono wako sasa na useme, “Nitafanya hivyo... Niombee, Ndugu Branham.” Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hakika Yeye atakufanya jambo hilo.

²⁵⁸ Baba yetu wa Mbinguni, katika Nuru ya Neno Lako, katika nguvu za kufufuka Kwako! Nami ninatambua, Bwana, ya kwamba maskini watu mara nyingi wanavurugwa huku nje, kwa mambo mbalimbali. Karibu watu hawajui la kufanya; mmoja anakuja, akisema jambo moja; na mwingine anakuja, akisema jambo lingine.

²⁵⁹ Na hapa katika Phoenix, jiji hili kuu la—la, vema, watalii, ambapo kila kitu kutoka kote nchini huchukuliwa kuingizwa humo, kimwili na kiroho pia. Nikisimama huko mlimani, hivi majuzi, na kuwazia ni mara ngapi Jina la Mungu linatumwiwa

bure katika siku moja hapa chini, kwamba ni uzinzi kiasi gani unaofanywa, ni dhambi ngapi na uchafu humu mitaani, na kwenye baa na walevi, na kila kitu, wengi wao wakidai kuwa ni waaminio, Wakristo!

²⁶⁰ Wanawake wakashuka kwenda barabarani, wameshika sigara mkononi mwao. Wakitembea huku wamevaa nguo za kitongozi, wakati Wewe ulisema zinanuka mbele Zako, "Ni chukizo," kama msalani wa kale mchafu, wenye kinyaa, unaonuka, mahali fulani. Ee Mungu, mwanamke anayedai kwamba ana Roho Mtakatifu angewezaje kufanya jambo kama hilo, na anajua ya kwamba katika pua ya Mwokozi, hizo zinanuka hivyo, uvundo? Angewezaje kuwa na kitu kama hicho katika Ufalme Wake? Baba, laiti wangalijua, wako maili milioni moja kutoka kwenye Huo.

²⁶¹ Ninaomba, Mungu, uturehemu. Hakuna mtu anayetaka kushuka kwenda kwenye nchi hiyo ya waliopotea. Hakuna mtu anayetaka kwenda kule, Baba. Na iwe mbali na yeote wetu kwenda. Hata hivyo kule chini kuna moyo mzuri katika mtu huyo, mwanamume huyo, mwanamke huyo, mwanamume ama mwanamke ambaye ni mwenye fadhili na mzuri na mwema, naye amedanganywa tu na ibilisi. Ibilisi amefanya jambo hilo.

²⁶² Shetani, ninakupinga, kwa sababu wewe ni adui wa Bwana wangu. Wewe ni adui wa Neno Lake. Nami ninakuamuru, kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kama mwanadamu, nikijua ya kwamba sina nguvu ndani yangu. Sina nguvu za kukuzuia. Sina nguvu za kumfanya yeote wa wanawake hawa kujisafisha, yeote wa wanaume hawa, wanaosikiliza kanda hii, ama—ama popote pale. Sina njia ya kuwafanya wajisafishe. Sina nguvu. Bali nina mamlaka ya Neno la Mungu, kama mtumishi, kulihubiri, na ninawajibika kwa mamlaka hayo. Wala polisi huyu hapa nje hana nguvu ya kusimamisha gari, bali ana mamlaka ya kulismamisha.

²⁶³ Na, Shetani, afadhali uanze kufunga breki zako, maana ninakuamuru, kwa Yesu Kristo, kwamba uwaachilie watu hawa, kote ulimwenguni, popote Ujumbe huu unapoweza kwenda. Waachilie. Ninawadai, kwamba wamenunuliwa. Wao si mali yao wenywewe. Wamenunuliwa kwa thamani, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, Bwana Yesu.

²⁶⁴ Ewe mnafiki mchafu, mwenye kinyaa, unayenuka, mwenye kuwadanganya wanadamu, ukiwaongoza bila wao kufikiri kuwaingiza katika handaki za kuzimu, waachilie. Ninakuamuru, kwa Mungu aliye hai, kwa Dhabihu ya Mwanawewe, Yesu, kwamba uwaachilie, kusudi nafsi zao zizazwe baraka Zake na Uwepo Wake, wapate kumiliki mlango wa kila adui. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Unawafanya wangojee *hiki, kile*, ama *kinginecho*, ama mguso fulani mtakatifu, ama kitu kingine, bali ninasema utawaachilia.

²⁶⁵ Magonjwa yangewezaje kustahimili upako kama huu? Ni wakati tu wanapokataa kuangalia huko ng'ambo kwenye ahadi kama baba Ibrahimu alivyofanya, wakati angaliweza kumwona katika mfano umbali wa mamia ya miaka, akiija.

²⁶⁶ Waachilie. Katika Jina la Yesu Kristo, achilia hao watu waondoke.

²⁶⁷ Jalia nguvu za Mungu, ufahamu wa Neno, wanaposafishwa asubuhi ya leo Nalo, jalia ufahamu wa kushikilia Neno la Mungu na ahadi Zake ambazo ni kweli, msimamo ambao hauwezi kuvunjwa na Shetani. Jalia kila mmoja ashikilie ahadi hiyo, akisema, “Hii ndiyo. Ninaishikilia. Mungu alifanya ahadi. Mimi ni uzao wa Ibrahimu. Ninawezaje kushuku ahadi Yake?” Na asonge mbele moja kwa moja, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. Amina.

Nampenda . . .

²⁶⁸ Limekuwa likikata asubuhi ya leo, enyi marafiki. Hebu na tuabudu sasa kwa utamu.

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²⁶⁹ Ingewezeckana, si la kukufuru, hasha . . . Hili ni—ni la kidini. Na tumwinulie mikono Yeye tunayempenda. Na kusema:

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²⁷⁰ Sasa, kwa kila mwanamke ama msichana humu ndani, huu ni mkono wangu. Mungu anakupenda. Kwa kila mwanamume ama mvulana humu ndani, Mungu anawapenda. Ninawapenda. Sasa, siwezi kunyosha na kushika kila mmoja wa mikono yenu, bali Mungu na awaelezee kile ninachomaanisha. Tunapouimba huo tena, geuka tu na umpe mkono mtu fulani. “Hivi watu wote watajua ya kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu, mnapopendana, ninyi kwa ninyi.” Mimi . . .

Alinunua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²⁷¹ Hivi hamumpendi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hisi hiyo tamu ya Roho Mtakatifu! Neno ni hatua ya kusafisha, hukusugua tu kabisa, hukufanya kiumbe kipyga, huondolea yote mbali. Neno ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, linatahiri, likikatilia mbali mambo yote ya ulimwengu. Unaona?

Ndipo tunajisikia safi, tunesuguliwa kabisa, tunamkubali na kumwamini. Hivyo ndivyo jinsi tunavyoweza kuimba:

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²⁷² Huo ni mzuri? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ninaupenda tu kwa moyo wangu wote. Unaona? Hebu tuujaribu tena, kila mtu sasa, halisi, kwa sauti yako yote sasa.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.



Na UZAO WAKO UTAMILIKI MLANGO WA ADUI WAKE SWA62-0121M
(And Thy Seed Shall Possess The Gate Of His Enemy)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ultolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 21 Januari, 1962, katika Maskani ya Imani huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org